


PENGO KATI YA NYAKATI SABA

ZA KANISA NA ILE MIHURI SABA

 Habari za jioni, wapendwa. Ni—ni majaliwa makubwa kuwepo hapa tena katika nyumba ya Bwana, usiku wa leo, kuwa katika huduma, nami ningali ninakula ile—ile mana kutokana na asubuhi ya leo, ambapo nafsi zetu zilibarikiwa sana kwa Uwepo Wake mkuu. Na sasa, usiku wa leo, tunaninii . . . tunaanza somo la: *Pengo Kati Ya Nyakati Saba Za Kanisa Na Ile Mihuri Saba*.

² Nami nilikuwa tu nikizungumza, aduhuri ya leo, na rafiki mmoja. Na labda, Bwana akipenda, wakati fulani kwenye majira haya ya kiangazi, kama Yeye hatanichukua Nyumbani, ama—ama, nikirudi, nisipoenda ng'ambo ama cho chote kile, ningetaka kuingilia tena zile Baragumu saba za mwisho, unaona. Na yote yanaungana pamoja. Na—na halafu kuna yale Mapigo saba ya mwisho katika jambo hili. Na yote yanaungana kabisa pamoja, kama tutakavyoona wakati tunapoendelea.

³ Kwa hiyo, usiku wa leo, wakati tunapotulia kidogo . . . Huenda nikachukua muda mrefu kidogo usiku wa leo. Pamoja na hata . . . Mara nitakaporudi hapa, sasa . . . Kuhubiri kote nilikofanya huko Phoenix, sikupwelewa na sauti hata wakati mmoja, unaona. Hiyo ni kweli. Na, loo, jamani, jinsi nilivyohubiri kwa nguvu! Na kwa ninii, ninaamini, ilikuwa ni ibada ishirini na saba, bila ya kupwelewa kamwe na sauti. Lakini ni hali ya hewa tu hapa, unaona. Ni ninii tu, ni kwamba tu hapa si pazuri kiafya, ni bondeni kabisa. Ni hali mbaya tu ya hewa mahali hapa, na, kuhusu hali ya afya, mwajua, yale ninayomaanisha, ni—ni—ni pabaya. Na mhubiri ye yote ana . . . anayehubiri, hupwelewa na sauti, kwanza.

⁴ Rafiki yangu mmoja da—daktari aliniangalia ndani ya koo langu, wakati mmoja, aone kuna nini. Kasema, “Hakuna kitu.” Kasema, “Una sugu tu humo kwenye mishipa yako ya sauti.” Kasema, “Hiyo ni kutokana na kuhubiri.” Vema, kwa namna fulani ni—ni—ninapenda jambo hilo, wajua. Hilo lilinifanya nijisikie vizuri zaidi, mradi tu ingeweza kuhusishwa na kuhubiri, unaona. Lingekuwa ni sawa, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

⁵ Sasa, huenda tusiweze kupata katika miili yetu alama ya Ye . . . ya Yesu Kristo, kama vile alivyopata Paulo, kwa kupigwa. Lakini huenda tukapata alama yetu kutokana na kuhubiri na kutoa sauti yetu dhidi ya mambo yaliyo mabaya. Kwa hiyo,

tunashukuru ya kwamba haitubidi kupigwa tena, zaidi sana hadi kufikia wakati huu. Kwa hiyo sisi—sisi tunaninii . . .

6 Ni wangapi humu ndani wamesoma *Ni Wakati Gani, Mabwana?* Ama, wameusia, wajua, *Ni Wakati Gani, Mabwana?* Huo ulinifadhaisha kidogo. Kama hujausia, natamani kwa namna fulani, kama ungeweza kuusikiliza, ama kwa namna fulani. Ulinifadhaisha kwa namna fulani. Nilitaka tu kusema jambo hili kabla ya kuanza ibada. Mnamo—mnamo juma moja ama siku kumi zilizopita, nilifadhaika sana. Nilinini tu . . . Si—si—sikuninii tu, nisingendesha ibada au cho chote kile, kwa sababu si—sikujua ni nini. Iionekana kama kwamba lingeweza kuwa ni jambo lililokuwa baya, nami sikujua tu lilikuwa ni nini. Kwa hiyo nikaninii . . .

7 Asubuhi moja na mapema, niliamka, kwenda kwenye Magenge ya Sabino. Ambayo, kutoka nyumbani, ni kama tu dakika thelathini kwa gari kufikia kwenye . . . ama arobaini, kufikia kwenye kilele cha Magenge ya Sabino, halafu kuna njia inayoenda maili thelathini kupanda mlimani.

8 Nchi ya ajabu, kule juu. Ninaweza kuwa hapa jangwani, ambapo ni themanini na tisini, sasa hivi, na katika dakika thelathini niwe kwenye futi nane za theluji, unaona, juu kabisa mlimani. Tulikuwa huko Phoenix, hivi majuzi tu, ambako ilikuwa ishirini na kitu, nyuzi joto ishirini na nane. Walipasha moto kisima cha kuogelea, na watu walikuwa wanaogelea. Na yapata dakika arobaini kutoka hapo kwa gari, ilikuwa arobaini chini ya sufuri, huko Flagstaff. Unaona? Hiyo ndiyo tofauti iliyopo kutoka kwenye pepo nyepesi za milimani na jangwa. Na hali hiyo ya hewa ni nzuri sana kwa wenye ugonjwa wa pumu, na kadhalika.

9 Lakini, basi, nilipanda juu kwenye yale magenge, nami nilipanda huko juu sana nilivyoweza kupanda. Na ni—ni—nikamwuliza Bwana, wakati nikiwa nimeketi kule juu, mambo yote haya maana yake ni nini, na kadhalika. Nilikuwa kidogo nimefadhaishwa, wala sikujua nifanye nini.

10 Na kwa hiyo nilipokuwa nikiomba; jambo la ajabu lilitukia. Na—na—nataka kuwa mwaminifu. Sasa, ingewezekana kwamba nililala usingizi. Huenda ilikuwa ni kitu kama njozi, ama ingeweza kuwa ilikuwa ni o—o—ono. Zaidi sana ninaegemea kwenye kuamini kwamba lilikuwa ni ono. Kwamba, nilikuwa nimeinua mikono yangu juu, nikisema, “Bwana, mlipuko huu unamaanisha nini? Na malaika hawa saba katika kundi la—la piramidi, kunitwaa mimi juu toka ardhini na wakaeleka mashariki, inamaanisha nini?”

11 Nilikuwa nimesimama pale, nikiwa katika maombi, ndipo jambo fulani likatukia. Na, sasa, kitu fulani kilianguka kwenye mkono wangu. Nami najua, kama wewe hufahamu mambo ya kiroho, huenda likaonekana ni la ajabu sana. Lakini kitu fulani

kilianguka kwenye mkono wangu. Na, wakati nilipoangalia, ilikuwa ni upanga. Na mpini wake ulikuwa wa lulu, lulu nzuri kuliko zote nilizopata kuona. Na ile ki—kinga, mwajua, ambapo . . . Nadhani ni ya kuzuia mikono yako isichomwe, mwajua, wakati unapo- . . . wa—watu wakipigana; ilikuwa ni ya dhahabu. Na ubaba wa kitara chake haukuwa mrefu sana, lakini ulikuwa tu ni mkali kama wembe; na ulikuwa wa fedha imetayo. Nao ulikuwa ni kitu cha kuvutia kuliko vitu vyote nilivyowahi kuona. Ulinienea mkononi mwangu sawasawa kabisa. Nami nilikuwa nimeushika. Nikasema, “Jinsi ulivyo mzuri!” Nikauangalia. Nami nikawaza, “Lakini, unajua, siku zote ninaogopa upanga.” Kwa namna fulani nilifurahi ya kwamba sikuishi katika siku walipozitia, kwa maana ni—ninaogopa kisu. Na kwa hiyo ni—nikawazia, “Ningefanya kitu gani na huo?”

¹² Na wakati nilipokuwa nimeushika, mkononi mwangu, Sauti kutoka mahali fulani ikasema, “Huo ni upanga wa Mfalme.” Na kisha ukaondoka.

¹³ Vema, ni—nilishangaa ilimaanisha nini, “‘Huo ni upanga wa yule Mfalme.’” Nami nikafikiri, “Kama ingalisema, ‘upanga wa mfalme *fulani*,’ huenda ingekuwa kwamba ningalifahamu. Lakini ilisema, ‘upanga wa *yule* Mfalme.’” Kwa hiyo huenda nisiliweke jambo hili sawa, lakini nikawazia, “Kuna Mmoja tu, aliye *yule* Mfalme, Huyo ni Mungu. Na upanga Wake ni *Hili*, ‘Kali kuliko upanga ukatao kuwili,’ unaona. ‘Na mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu. . . .’” Unaona? Nami ni—nikawazia. . .

¹⁴ Watu wawili wanaposhindana kwa kupigana kwa upanga, unaona, na kama ninavyofa- . . . Sifahamu hata neno moja juu yake, lakini, au kanuni moja ya kushindana kwa upanga. Lakini, kwa fahamu zangu zote, kisu hicho kikipiga kwa kuingama. Na halafu, hatimaye, hizo—hizo panga, kama zikishikamana, wewe na adui mshikamanishe mapanga, namna *hii*, basi inatakiwa nguvu za mtu huyo anayeshindana. Kwa sababu, unaona, upanga wake utakuwa umeelekezwa kwenye moyo wangu, na wangu kwenye moyo wake, lakini panga hizo zimeshikana, kama vile visu vyetu vikigongana. Na ndipo wanapigana, halafu panga zinakutana. Na yule anayeweza kumsukuma mwingine chini, huo upanga umeelekezwa moja kwa moja moyoni. Kwa hiyo inatakiwa ninii. . .

¹⁵ Hata ingawa huo upanga ni Neno, inatakiwa mkono wa imani wenye nguvu kuushikilia pale, kuufikisha kwenye moyo wa adui. Sasa, bila kujua mambo haya, lakini ninii tu. . . Yote ambayo nimepokea kutoka Kwake, ambayo ninaweza kusema, nimewaambia. Kwa hiyo, hilo, mwajua, ninaamini lilikuwa ni ninii. . . Je! haikuwa ni Bwana wetu aliyesema, yote aliyokuwa amepokea kwa Baba, ya kwamba aliyasema, wala hakuacha kitu? Na—na kwa hiyo tunataka kufanya mambo hayo jinsi vile tu yanavyokuja. Sasa, kama mtakuwa wenye

hekima kweli kweli, na kuomba, nina hakika mtafahamu jambo fulani hivi karibuni sana, sasa, jambo fulani ambalo ninatumaini limefunuliwa.

¹⁶ Sasa, katika Kitabu hiki, hebu na tufungue sote kwenye—kwenye sura ya 5 ya Kitabu kinachoitwa Ufunuo wa Yesu Kristo.

¹⁷ Sasa, kesho usiku ni Muhuri wa Kwanza. Ambayo, Mihuri minne ya kwanza inafunguliwa, na wapanda farasi wanne, mmoja kwa kila muhuri unaokuja duniani. Na halafu, labda, haitakuwa ni mirefu, mpaka baada ya sisi kupita mnamo . . . Jumatatu, Jumanne, Jumatano, mnamo Alhamisi. Na halafu, nadhani, kwenye wa Sita . . . na wa Tano, wa Sita, na Muhuri wa Saba, huenda ikawa ni mirefu sana. Kwa hiyo, labda itawapa muda kidogo wa kupumzika kidogo.

¹⁸ Tunakusudia kuanza ibada hapa, ninaamini, kwenye saa moja, juma hili usiku. Nami ninapaswa kuwa jukwaani saa moja na nusu, kamili. Ndipo basi hiyo inaweza kutufanya tutoke kwenye usiku wa manane. Kwa hiyo—kwa hiyo, ni— nilipitisha saa moja, asubuhi ya leo. Sikukusudia jambo hilo, nilininii tu . . . Sijui ni wakati gani.

¹⁹ Kwa sababu, sijui mpanda farasi wa kwanza ni nini. Sijui wa Pili, wa Tatu, wa Nne, wa Tano, wa Sita, ama Muhuri wa Saba. Mimi, hadi wakati huu, sijui. Mnaona? Ninamtegemea Yeye tu. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu, ninajaribu juma hili, kwa neema ya Mungu kusaidia, nikiamini ya kwamba, kama mnafahamu ninii kwa undani . . .

²⁰ Unajua, katika maono, huwezi kufunua mambo mpaka uruhusiwe kuyafunua. Ni mara ngapi ninyi nyote mmenisikia nikisema, “Unaingia kwenye nyumba fulani, labda kofia itakuwa imekaa *hapa*. Na mtoto huyu fulani, ama cho chote kile, hataponywa mpaka kitu kile kimewekwa *hapa*.” Siwezi kuwaambia, au wala mimi siwezi kuisogeza pale. Haina budi kuwa ninii, kusogezwa, kwa njia nyingine fulani. Mtu fulani mwingine hana budi kuichukua na kuisogeza. Na, kila kitu mahali pake, ndipo jambo linaweza kufunuliwa.

²¹ Kwa hiyo sasa iweni katika maombi. Sasa, kabla tu hatujakikaribia Kitabu hiki, hebu na tuzungumze Naye, huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

²² Bwana Yesu, sisi tu wapungufu kabisa. Tusingejaribu, kwa njia yo yote, kukikaribia Kitabu hiki kitakatifu, katika saa hii iliyo takatifu sana ambayo nafsi zinaning’inia katika kikomo cha wakati, bila ya kumwomba, Bwana, huyo, Yeye Huyo ambaye ndiye tu anayeweza kukifunua Kitabu hiki, ya kwamba aje sasa, kubariki jitihada hafifu za mtumishi Wako. Bariki Neno wakati linapotoka. Naomba liende katika nguvu za Roho. Na jalia msingi wa kiroho wa . . . wale wanaoona njaa na kiu ya kujua haki na kujua mapenzi ya Mungu, jalia liangukie kule ndani na lizae kwa jinsi Yake. Tujalie, Bwana. Sifa zote na ziwe

Zako. Jalia wenye njaa na kiu wapate chakula na kinywaji, usiku wa leo, kutoka kwenye Neno. Tunaomba katika Jina la Yesu, Ambaye huu ufunuo ni wake Yeye. Amina.

²³ Basi, sasa tutafungua kwenye sura ya 5. Sasa, hii si ile Mihuri Saba. Ni lile pengo kati ya nyakati za kanisa na Mihuri Saba. Sasa, pia kuna sura ya 6 ya . . .

²⁴ Na kulikuwako na sura ya 4, hasa, ya Ufunuo, na, katika hiyo, kwa namna fulani ilifunua jambo fulani litakalotukia baada ya kunyakuliwa kwa Kanisa. Kwamba, kanisa linanyakuliwa katika sura ya 3 ya Ufunuo, na halirudi mpaka sura ya 19 ya Ufunuo. Mnaona? Kwa hiyo, kanisa haliingii katika ile Dhiki. Ninajua jambo hilo ni kinyume cha—cha karibu kila mwalimu niliyepata kuzungumza naye. Lakini si—si—sitaki kuhitilafiana. Ni—ninataka kuwa ndugu yenu, lakini si—sina budi kufundisha jinsi tu ninavyoweza kuliona. Kama sifundishi hivyo, siwezi kuliunganisha pamoja, mnaona. Na sasa, iwapo linanyakuliwa kabla ya ile Dhiki ama baada ya ile Dhiki, ninataka kunyakuliwa pamoja Nalo. Hilo ndilo jambo muhimu.

²⁵ Kwa hiyo, mambo hayo tu—tunayadhania tu, kwa maana, bila elimu, mimi hufundisha kwa mifano. Ninaangalia na kuona mambo yalivyo, ama jinsi yalivyokuwa katika Agano la Kale, ambalo ni mfano ama kivuli cha lile Jipya, ndipo ninapata fununu jinsi lile Jipya lilivyo. Mnaona? Kama vile. . . Nuhu aliingia safinani kabla ile dhiki haijaanza, mfano, lakini hata kabla ya Nuhu, mnaona, kuingia safinani, Henoko alinyakuliwa, unaona, kabla halijatukia jambo lo lote. Naye Lutu aliiitwa atoke Sodoma kabla chembe moja ya dhiki kuanza, ya maangamizi; lakini Ibrahimu alikuwa, wakati huo wote, nje ya jambo hilo. Unaona, mifano.

²⁶ Lakini sasa tutasoma aya ya 1. Nitasoma aya za kwanza mbili ama tatu Zake.

Kisha nikaona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi kitabu kilichoandikwa ndani na nyuma, kimetiwa muhuri saba.

Nikaona malaika mwenye nguvu akihubiri kwa sauti kuu, Nnani astahiliye kukifungua kitabu, na kuzivunja muhuri zake?

Wala hapakuwa na mtu mbinguni, wala juu ya nchi, wala chini—wala chini ya nchi, aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama. (Ni Kitabu cha ajabu jinsi gani!)

Nami nikalia sana kwa kuwa hapakuonekana mtu astahiliye kukifungua na kukisoma hicho kitabu, wala kukitazama.

27 Sasa, unanena kuhusu kutostahili? “Hata kustahili kukitazama; hapana mtu, mahali po pote.”

Na mmojawapo wa wale wazee akaniambia, Usilie; tazama, Simba aliye wa kabila ya Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na zile muhuri zake saba.

Nikaona, na, tazama, katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne, . . . katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote.

Akaja, akakitwaa kile kitabu katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi.

28 Tutasimama hapo kwa muda kidogo, katika kusoma Ufunuo sura ya 5, kuendelea hata kufikia aya ya 7.

29 Kitabu hiki cha Mihuri Saba kinafunuliwa wakati wa zile Ngurumo Saba za Ufunuo 10, sasa, kama unayaandika. Hebu na tufungue Ufunuo 10, kwa muda kidogo tu, kusudi mpate kuelewa kabla hatujalifikia. Sasa, huu ni wakati wa mwisho. Kwa maana, sikilizeni:

. . . nikaona malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni, amevikwa wingu; na upinde wa mvua . . . juu ya kichwa chake; . . .

30 Kama ukiangalia, huyo ni Kristo, unaona. Maana, Yeye, katika Agano la Kale, aliiitwa Malaika wa Agano. Naye anakuja moja kwa moja kwa Wayahudi sasa, kwa maana Kanisa limekwisha. Unaona? Vema.

. . . na uso wake . . . kama jua, na miguu yake kama nguzo za moto.

31 Mnamkumbuka yule Malaika katika Ufunuo 1? Jambo lile lile. Malaika ni “mjumbe.” Naye ni Mjumbe kwa Israeli. Mnaona? Kanisa limekwisha kunyakuliwa, mnaona, sasa, ama linakaribia kunyakuliwa. Yeye anakuja kwa ajili ya Kanisa Lake. Sasa angalia.

Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa . . .

32 Sasa, hapa, kilikuwa kimefungwa hapa na kutiwa muhuri; na hapa kimefunguliwa. Kimefunguliwa. Tangu wakati huo wa kutia muhuri, tutakaofikia usiku wa leo, sasa hicho Kitabu kimefunguliwa. “Kitabu kidogo mkononi Mwake, katika ninii Yake . . . Kilikuwa kimefunguliwa. Loo, jinsi jua, kama nguzo . . .” Ngoja kidogo tu. Hebu nianzie hapa nyuma na kusoma.

Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa. Akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi.

Naye akalilia kwa sauti kuu, kama simba angurumavyo: . . .

33 Tunajua Yeye ni Simba wa kabila ya Yuda. Hapa Yeye ni Mwana-Kondoo; lakini hapa Yeye ni Simba. Unaona?

. . . Na alipolia, zile ngurumo saba zikatoa sauti zao.

34 Sasa, Yohana aliagizwa kuandika aliyoona, kwa hiyo mtume huyo, na nabii, akatwaa kalamu yake kuandika Hayo.

Hata ngurumo saba zilipotoa sauti zao, nalikuwa tayari kuandika. Nami nalisikia sauti kutoka mbinguni ikiniambia, Yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo ngurumo saba, usiyaandike.

35 Sasa, hayo ndiyo ambayo hatujui. Hayo bado ni mambo ya kufunuliwa. Hayamo katika Maandiko Matakatifu, yale yanayosemwa na hizo Ngurumo.

Na yule malaika niliyemwona, akisimama juu ya bahari na juu ya nchi, akainua mikono yake kuelekea mbinguni, (sasa sikilizeni)

Ndipo akaapa kwa yeye aliye hai hata milele na milele, yeye aliyeziumba mbingu na vitu vilivyomo, na nchi na vitu vilivyomo, na . . . hapatakuwa na wakati baada ya haya;

36 Angalia! Hii hapa aya ninayotaka kuifikia.

Isipokuwa katika siku za sauti ya malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi wake hao manabii.

37 Sasa, angalia, siri ya Kitabu hiki cha Mihuri Saba itafunuliwa wakati wa kupigwa baragumu ya Ujumbe wa malaika wa kanisa la saba. Unaona? “Malaika wa saba anaanza kupiga baragumu,” na ndizo hizo hapo Jumbe zilizoandikwa humo, nasi tunazo kwa jinsi ya kanda na vitabu. Sasa, “Mwanzoni mwa kutangazwa kwa Ujumbe huo, siri ya Mungu itamalizika, unaona, wakati huo.” Sasa tutaona. Kile Kitabu, cha siri ya Mungu, hakifunuliwi mpaka Ujumbe wa Malaika wa saba utakapotangazwa.

38 Sasa, mambo haya yatakuwa ni muhimu katika ile Mihuri, nina hakika, maana hakina budi, kwa kila sehemu, kushikamana.

39 Sasa, kimeandikwa kimafumbo, kwa sababu hakuna mtu, mahali po pote, anayekijua. Mungu peke Yake, Yesu Kristo, unaona. Sasa, lakini ni . . . Ni Kitabu, Kitabu cha kimafumbo. Ni Kitabu cha Ukombozi. Tutaingilia jambo hilo, hivi punde.

Na sasa tunajua ya kwamba Kitabu hiki cha Ukumbozi hakitafahamika vizuri kabisa; kimechunguzwa, katika nyakati sita za kanisa. Lakini mwishoni, wakati malaika wa saba atakapoanza kutangaza siri yake, anamalizia sehemu zote zilizoachwa ambazo jamaa hawa walichunguza. Nazo hizo siri zinashuka kutoka kwa Mungu, kama Neno la Mungu, na kufunua ufunuo wote mzima wa Mungu, ndipo Uungu na cho chote kile kinakamilishwa. Siri zote, uzao wa nyoka, na cho chote kile, zitafunuliwa.

⁴⁰ Sasa, unaona, mimi sijibunii tu jambo hilo. Hivyo ndivyo. . . Ni BWANA ASEMA HIVI. Nitawasomea Hilo kutoka katika Kitabu, “Kule kutangazwa kwa Ujumbe wa malaika wa saba, siri ya Mungu itatimizwa, ambayo imetangazwa na manabii Wake watakatifu,” hao ni manabii walioliandika Neno. Wakati wa kutangazwa, kwa ule wakati wa saba wa kanisa, ule wakati wa mwisho wa kanisa, sehemu zote zilizoachwa, ambazo zimechunguzwa-chuguzwa katika nyakati hizi za kanisa, zitamalizwa.

⁴¹ Na wakati ile Mihuri inapovunjwa, na ile siri imefunuliwa, yule Malaika anashuka, yule Mjumbe, Kristo, akiweka mguu Wake juu ya nchi na juu ya bahari, akiwa na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake. Sasa, kumbukeni, malaika huyu wa saba yuko duniani wakati wa Kuja huku.

⁴² Kama tu vile Yohana alivyokuwa akitoa ujumbe wake, wakati uo huo ambao Masihi alikuja katika siku hizo. Yohana alijua angemwona Yeye, kwa maana angekuja kumtambulisha.

⁴³ Nasi tunatambua ya kwamba, katika Maandiko, katika Malaki 4, kutakuwako na mtu kama Yohana, E—Eliya fulani ambaye Neno la Mungu linaweza kumjia. Naye atafunua, kwa Roho Mtakatifu, siri zote za Mungu, na kuirudisha Imani ya watoto ielekee imani ya baba zao mitume, arudishe siri hizo zote ambazo zimechunguzwa-chunguzwa, katika miaka hii ya kimadhehebu. Sasa, hivyo ndivyo Neno lilivyosema. Mimi ninahusika tu na vile lilivyosema. Unaona? Imeninii, imeandikwa, ni kweli. Hivyo ndivyo lilivyo.

⁴⁴ Sasa, tunaona ya kwamba Kitabu hiki cha Mihuri Saba, sasa, ni siri ya ukombozi. Ni Kitabu cha Ukombozi, kutoka kwa Mungu.

⁴⁵ Sasa, siri zote, kwenye wakati huu, zitatimizwa wakati mjumbe huyu anapopiga baragumu. Sasa, *hapa* pana malaika duniani; na Malaika “mwingine,” Mjumbe mwenye nguvu, anashuka. Unaona, malaika *huyu* alikuwa ni malaika wa duniani, mjumbe; lakini *hapa* anashuka Mwingine kutoka Mbinguni, agano la upinde wa mvua, unaona, angeweza tu kuwa ni Kristo.

⁴⁶ Kama tu vile ilivyokuwa kabisa katika Ufunuo, sura ya 1, “Amesimama katikati ya Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu,

akiwa na upinde wa mvua, akionekana mithili Yake kama jiwe la yaspi na akiki.”

⁴⁷ Naye huyu hapa anarudi, katika sura ya 10, baada ya wakati ule wa kuja ambapo siri zote zitatimizwa na Mihuri itavunjwa, na kutangazwa ya kwamba, “Hapatakuwa na wakati baada ya haya.” Naye akasema, “Wakati malaika wa saba atakapoanza kupiga baragumu, basi siri haina budi kutimizwa, na ni wakati wa Malaika huyo kutokea.” Tuko karibu, mahali fulani. Vema. Sasa angalia.

⁴⁸ Zile Muhuri Saba zinashikilia ile siri ya Kitabu hicho. Mpaka tutakapoweza kuona ni kitu gani hiyo Mihuri Saba imefungia humo ndani, tunadhania tu mambo hayo. Kwa sababu, kama nilivyokwisha kuwaambia, asubuhi hii, juu ya Ujumbe wangu mdogo asubuhi ya leo, wa Mungu akijificha katika urahisi. Mnaona, tu—tuna . . . Hakika tutapitwa na jambo hilo isipokuwa liwe limefunuliwa kabisa, limefunuliwa kweli na Roho Mtakatifu, na kuthibitishwa vivyo hivyo. Unaona? Kama nabii akiinuka na kukwambia ya kwamba Hili ndio Lile, na Mungu asithibitishwe vivyo hivyo, sahai. Unaona? Lakini Mungu, katika kila tamshi, katika kila kitu, hana budi kulithibitisha, kulifanya kuwa sahihi. Unaona? Kwa hiyo, watoto Wake watayaangalia mambo hayo, unaona, na kuwa macho, angalia.

⁴⁹ Mihuri Saba kwenye Kitabu hicho, zime-. . .Muhuri hizi Saba zimekifunga Kitabu hiki. Unaona? Kitabu hiki kimefunguwa kabisa. Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kitabu hiki ni Kitabu kilichofungwa kabisa mpaka ile Mihuri Saba itakapovunjwa. Kimefungwa kwa Mihuri Saba. Sasa, hiyo ni tofauti na zile Ngurumo Saba. Unaona? Hizi ni Muhuri saba kwenye kile Kitabu. Nacho Kitabu hakitaninii, Mihuri haitaachiliwa mpaka kwenye ule Ujumbe wa malaika wa saba. Unaona? Kwa hiyo tuna—tunadhania; lakini ufunuo halisi wa Mungu utakamilishwa katika kule kutangazwa kwa ile Kweli iliyothibitishwa. Sasa, hivyo ndivyo Neno linavyosema hasa, “Ile siri itatimizwa katika wakati huo.”

⁵⁰ Na Kitabu hiki cha Mihuri Saba, kumbuka, kilikuwa kimefungwa hapa, katika Ufunuo sura ya 5, na katika Ufunuo sura ya 10 kimefunguliwa.

⁵¹ Na sasa tutaona vile Kitabu hiki kinavyosema kuhusu jinsi kilivyofunguliwa. Na hakijulikani mpaka Mwana-Kondoo anapokitwaa kile Kitabu, na kuivunja ile Mihuri, na kukifungua Kitabu. Mnaona? Mwana-Kondoo hana budi kukitwaa kile Kitabu.

⁵² Kimefichwa. Sasa kumbukeni, “Hakuna mtu Mbinguni, hakuna mtu duniani,” papa, askofu, kadinali, mzee wa jimbo, ama ye yote yule, “anayeweza kuivunja hiyo Mihuri, wala kukifunua kile Kitabu, ila Mwana-Kondoo.” Nasi tumetafuta,

na kubahatisha, na kujikwaakwaa, na kushangaa, na—na hiyo ndiyo sababu sote tuko katika mchafuko kama huu.

⁵³ Lakini tukiwa na ahadi ya Kiungu ya kwamba Kitabu hiki cha Ukumbozi kitafunguliwa kikamilifu na Mwana-Kondoo, na Mihuri yake itafunguliwa na Mwana-Kondoo, katika siku za mwisho tunazoishi sasa. Na hakitajulikana mpaka Mwana-Kondoo atakapokitwaa Kitabu hicho na kuivunja ile Mihuri. Kwa sababu, kumbukeni, kile Kitabu kilikuwa kimeshikiliwa katika mikono ya Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi. “Naye Mwana-Kondoo anamjia Yeye aketiye juu ya Kiti cha Enzi, na kukitwaa kile kitabu kutoka katika mkono Wake wa kuume.” Anakitwaa kile Kitabu! Loo, hilo ni la kilindi. Tutajaribu kulitatua kama tukiweza, kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Sasa tunamtegemea Yeye. Nasi tutaona, baadaye, ni kwenye wakati wa mwisho, “Hapo wakati utakapokuwa umekwisha.”

⁵⁴ Hakuna madhehebu yaliyo na haki ya kukifasiri Kitabu hiki. Hakuna mtu aliye na haki ya kukifasiri. Mwana-Kondoo ndiye anayekifasiri. Na Mwana-Kondoo ndiye anayekinena, naye Mwana-Kondoo analifanya Neno lijulikane, kwa kulithibitisha na kulihuisha Neno. Unaona? Kweli kabisa! Angalia. Nacho hakifunuliwi mpaka . . .

⁵⁵ Kitabu hiki hakifunuliwa mpaka nyakati za kanisa na nyakati za kimadhehebu zimekwisha, “na hapana wakati tena.” Unaliona? Kinafunuliwa tu baada ya nyakati za kanisa na nyakati za kimadhehebu kwisha.

⁵⁶ Hiyo ndiyo sababu jambo hilo liko kwenye utata hivyo usiku wa leo. Unaona, wao wanachukua fundisho duni, na kwenda nalo *hapa* upande mmoja, waseme, “Hii ndiyo Kweli!” Mwingine anaokota fundisho lingine, anakimbilia upande *huu*, kasema, “Hii ndiyo Kweli!” Na kila mmoja anaunda madhehebu chini ya kitu hicho, mpaka tuna mamia ya madhehebu. Lakini hata hivyo, katika hayo yote, kuona ule mchafuko, watu wanashangaa, “Kweli ni nini?” Kama hiyo siyo sawasawa na hali ilivyo ya siku hizi!

⁵⁷ Lakini basi Yeye anaahidi, ya kwamba, “Hapo wakati wa jinsi hiyo utakapokwisha, kutakuwako na kutangazwa kwa sauti ya malaika wa saba, na ndipo kile Kitabu kitafunuliwa, unaona, katika wakati huo.”

⁵⁸ Sasa, msiseme, mtu ye yote asiseme, “Hao watu nyuma kule hawakuokoka.”

⁵⁹ Lakini, zile siri, ambazo hawakuweza kufahamu! Jinsi ambavyo Mungu anavyoweza kuwa watatu na, hata hivyo, ni Mmoja! Jinsi ambavyo Maandiko yanavyoweza kusema, “Mkabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” na kugeuka tena na kusema, “Mkabatize katika Jina la Yesu.” Unaona? Loo, mambo mengi sana! Hawa anawezaje kula tofaa na asababisha ma—maangamizi ya ulimwengu mzima? Unaona?

Mambo haya yanawezekanaje? Lakini siri hizo zimeahidiwa kufunuliwa katika wakati wa mwisho.

⁶⁰ Ni mambo madogo, yaliyoachwa ambayo. . . Mashujaa hawa wakuu wametokea jukwaani, kama vile Ireneo, na Martin, Mtakatifu Martin, na Polikapu, na watu mbalimbali, na Luther, na Wesley, na hawa wote. Unaona? Jinsi wamekuja na kuishi tu muda mrefu wa kutosha ku—kuleta nuru kwa namna fulani na kuiangaza, lakini waliacha mambo mengi katika—katika giza. Ndipo ukaja Wakati wa Pentekoste, kama Wakati wa Kilutheri, nao wakaishia kwenye utata. Lakini bado, vema, usiseme hawakuwa sahihi. Walikuwa sahihi. Lakini kuna vitu vilivyoachwa vimelegea, ambavyo haviwezi kuelezewa. Lakini basi katika. . . Kwa nini? Mihuri haijavunjwa, ipate kufunua kikamilifu mambo haya ni nini. Unaona?

⁶¹ Lakini basi, katika wakati wa mwisho, siri hizi zote hazina budi kutatatuliwa na kutolewa. Na hiyo Mihuri itafunguliwa na Mwana Kondoo, na kufunuliwa kwa Kanisa, ndipo hapatakuwa na wakati baada ya haya. Unaona? Ni ajabu jinsi gani! Basi, kile Kitabu, basi, ni Kitabu Cha Ukombozi. Kwa kuwa, halafu kinaendelea mbele. . .

⁶² Na tutaingiza, baadaye, jinsi wale mia na arobaini na nne elfu wanavyoingizwa, na kadhalika. Vema. Hao ni Wayahudi.

⁶³ Sasa, sasa, Paulo. Hebu na tusome kidogo. Napata baadhi ya Maandiko haya, nami ninafikiria tunapaswa ku—kuyasoma. Sasa hebu sote na tufungue; Paulo, katika Waefeso 1.

⁶⁴ Wengi wao naona wanaandika. Wana vitabu vyao na wanaandika Maandiko, wakiyatilia alama katika Biblia zao, kwa ajili ya kuunganisha. Kwa hiyo, hilo—hilo ni jambo zuri. Ninawataka mfanye hivyo, kisha mwende nyumbani mkajifunze Hilo. Mnaona? Na—na ukijifunza hilo, wewe mwenyewe, ndipo uta—utalifahamu vizuri zaidi. Unaona? Lisome tu Hilo, na umwombe Mungu akusaidie kufahamu.

⁶⁵ Sasa hebu na tusome A—Andiko nililoandika hapa chini. Waefeso 1:13 na 14, sasa.

Nanyi pia katika huyo tumetumaini baada ya kulisikia neno la kweli, na habari njema za wokovu wenu; katika yeye. . . baada ya kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.

Ndiye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake. Mnaona?

⁶⁶ Sasa, wakati tumefungua Maandiko, hebu tuninii. . . Mnaona, Roho Mtakatifu hapa, Mwenyewe, ni Muhuri. Roho Mtakatifu ni Muhuri. Na Muhuri unaonyesha (kitu gani?) kazi iliyomalizika, Roho Mtakatifu akiwa ni Muhuri kwa mtu binafsi. Na kwa mtu huyo binafsi, wakati anapompokea Roho Mtakatifu,

basi wakati wake wa kuugua umekwisha, unaona, kwa sababu ni kazi iliyokamilika.

⁶⁷ Kwa mfano, nilikuwa ninafanya kazi katika shirika la reli, nasi tungepakia makopo kwenye mabehewa na vitu mbalimbali kutoka kwenye kiwanda cha kusindika vyakula vya makopo. Na, lakini, basi, kabla behewa hilo halijatiwa muhuri, mkaguzi alikuja pale, kuona kama behewa hilo lilikuwa limepakiwa vizuri. Kama halijapakiwa vizuri, [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] lilipoanza kugongana na kitu fulani tu, litasambaza vitu hivyo na kuvivunja, na—na shirika hilo la reli lingewajibika. Na mkaguzi huyo angehakikisha kila kitu, kuona kwamba kilikuwa kimekaa mahali pake sawasawa. Kama hakikukaa vizuri, yeye alilikataa behewa hilo. Basi ilitubidi kurudia kazi hiyo tena, mpaka yule mkaguzi aliporidhika. Na basi mkaguzi anapokuwa ameridhika, anafunga mlango. Mkaguzi anafunga mlango. Na mkaguzi huyo anaweka muhuri juu yake, na ndipo hakuna mtu anayeweza kuvunja muhuri huu mpaka litakapofika linakoenda.

⁶⁸ Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyokuwa akifanya. Unaona? Yeye huenda na kukagua. Hiyo ndiyo sababu hamwezi kupata mambo haya na . . . Unasema, “Nilinena kwa lugha, na nilipaza sauti, na nilicheza katika Roho.” Hilo halina uhusiano wo wote na jambo Hilo. Unaona? Roho Mtakatifu humkagua mtu huyo mpaka Yeye ameridhika kabisa na anajua ya kwamba wako sawa.

⁶⁹ Ndipo, wao wanatiwa muhuri mpaka kikomo chao cha Milele. Hakuna kitu kinachoweza kuvunja Muhuri huo hata kidogo. Biblia . . . Mnaandika Maandiko yenu. Waefeso 4:30, ilisema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mliwiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.” Shikilia neno hilo, “ukombozi,” unaona. Mpaka ile siku ambayo Kitabu cha Ukombozi kimefunuliwa, na Mkombozi anakuja na kudai mali Yake! Hakuna kitu kinachoweza kufanya jambo hilo. Unaona? “Msimhuzunishe.” Kaeni . . . Fanyeni mambo yanayompendeza Mungu, kwa kuwa Kitabu hicho kimetiwa muhuri, sasa, nanyi mmetiwa muhuri. Roho Mtakatifu, Mwenyewe, ndiye ule Muhuri.

⁷⁰ *Muhuri* unaonyesha . . . Sasa, haya ni maneno niliyopata kutoka katika kamusi. *Muhuri* huonyesha “kazi iliyokamilika.” Na wakati ule Muhuri wa Saba utakapovunjwa, ile siri ya Mungu iliyotiwa muhuri katika Mihuri hii ya siri imekwisha. Mpaka ile siku ambapo Muhuri huo utakapovunjwa, halafu kile kilicho ndani Yake kinafunuliwa.

⁷¹ Kama mtu huyo anajiuliza ni kitu gani kilichoko ndani ya behewa hilo, aseme, “Kunapaswa kuwe na *kadha na kadha*. Kunapaswa kuwe na kitu.” Anadhania. Lakini wakati huo muhuri umevunjwa na mlango uko wazi, basi tunaona

yale yaliyoko ndani yake na kuona sawasawa kile kilichoko mle ndani.

Unaona? Na jambo hilo litafanyika tu katika wakati wa mwisho.

⁷² Jambo lingine Muhuri unaloonyesha, ni “umilikaji.” Unaona, Muhuri una alama juu Yake, unaonyesha umilikaji. Wakati wewe unaponunuliwa kwa Damu ya Yesu Kristo, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu, wewe si mali ya ulimwengu huu tena wala cho chote cha ulimwengu huu. Wewe ni mali ya Mungu.

⁷³ Jambo lingine, ni hili, Muhuri ni “usalama.” Muhuri unamaanisha wewe ni salama. Sasa, ninyi ambao hamwamini katika usalama wa Milele, sijui, unaona. Lakini sasa, lakini, Muhuri unaonyesha usalama mpaka kwenye kikomo cha kitu. Ole wake jamaa huyo ambaye angejaribu kuvunja Muhuri huo! Na Muhuri wa Roho Mtakatifu hauwezi kuvunjwa.

⁷⁴ Nyote mmenisikia nikisema ya kwamba watu walisema, “Ibilisi alinifanya nifanye jambo *hili*.” La, la, Ibilisi hakufanya jambo hilo. Wewe hukuwa tu umefungiwa ndani kwa kutiwa muhuri. Maana, wakati unapofungiwa ndani kwa kutiwa muhuri, yeye anafungiwa nje. Naam. Unaona? Sasa, wewe ulitoka ukamwendea. A-ha. Yeye hangeweza kuingia ndani yako, kwa sababu njia pekee ya kuingia ndani yako ni kupitia katika hatua zile zile ulizopitia. Ingembidi aokolewe, atakaswe, na kujazwa na Roho Mtakatifu, ndipo angekuwa ni ndugu yako. Kwa hiyo, unaona, kwa hiyo yeye—yeye hakufanya jambo hilo. La, la. Wewe ulienda tu ukafika mpakani kisha ukarudi, ukivitamani vitu vya ulimwengu. Hukwenda moja kwa moja mpaka Kanaani, unaona, ukavuka Yordani, kule kufa kwa nafsi yako. Unaona?

⁷⁵ Sasa angalia, sasa, Kitabu hiki kimetiwa muhuri. Na—nawe umetiwa muhuri, pamoja na Kitabu hicho, hata Siku ya Ukombozi.

⁷⁶ Tena, katika Warumi 8:22 na 23. Hebu na tufungue hiyo, nasi tutaweka msingi huu, ndipo nafikiri tutafahamu jambo Hilo vizuri zaidi kidogo kama kila mtu akijisomea mwenyewe. Ninawapa Maandiko machache hapa, kusudi tuweze—tuweze kuyaangalia Hayo, na wakati kungali ni mapema. Sasa, 8, Warumi 8:22, kuanzia.

Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa.

Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu.

77 Loo, jamani! Loo, jamani! Je! hilo halitufanyi sisi wazee kujisikia vizuri? Linapaswa kutufanya sisi sote kuwa na furaha, tukiingojea saa hii. Tunafahamu ya kwamba jambo hili litatukia katika ule ufufuo wa kwanza. Unaona? Viumbe vinaugua. Tunaugua. Kila kitu kinaugua, kwa sababu tunatambua kuna kasoro fulani. Na jinsi tu unavyoweza kuugua, na kukiingojea, ni kwa sababu Uzima mpya umeingia *hapa* ndani, unaonena habari za Ulimwengu mpya.

78 Kama vile mke wangu hapa, si muda mrefu uliopita, tulienda hapa kwenye soko kuu. Nami nikasema, “Tuliona kitu cha ajabu; mama fulani alikuwa amevaa gauni.” Na lilikuwa ni jambo la ajabu mno, unaona. Wao, wao wananinii. . . Karibu wote hawavai magauni, unaona. Na, kwa namna fulani, wao ni wasahaulifu; wanatoka wanaenda bila nguo. Kwa hiyo basi sisi. . . Wao wanasahau makusudi.

79 Na kwa hiyo, basi, Meda akaniambia, akasema, “Bill, mbona inakuwa hivyo?” akasema.

80 “Loo,” nikasema, “ni roho tu ya taifa.” Tena nikasema, “Unapoenda Ujerumani, wao wana roho ya namna fulani. Nenda Finland, wao wana roho ya kitaifa. Ukija Marekani, tuna roho ya taifa.”

81 Roho ya taifa letu ni ya mizaha, utani. Mnajua ni kwa nini? Tulianza mwanzoni na Fundisho la mitume. Tulianza juu na uongozi wa watu mashuhuri, kama vile Washington, Lincoln. Lakini tumeondoka kwenye msingi huo, nasi tunajua ya kwamba tutajuta. Tunajua ya kwamba bomu la atomiki limeandikwa jina letu juu yake. Tunajua ya kwamba utumwa uko mbele zetu. Hakuna haja ya kujipumbaza.

82 Inanikumbusha, kama baadhi ya hawa wacheshi, wanaokwenda pale na—na kufanya vicheko vya mizaha hii, na kufanya vituko vyao, na wanawake wakifanya wanavyotenda, na wanaume, pamoja. Inanikumbusha tu juu ya mvalana mdogo aliyekuwa akipitia makaburini, huku akipiga mbinja, eti akijaribu kujifanya aamini kwamba haogopi. Hakika, anaogopa. Unaona? Yeye hampumbazi mtu ye yote. Hiyo ndiyo sababu anapiga mbinja. Unaona? Anajaribu kusema eti haogopi, lakini anaogopa. Na hivyo ndivyo ilivyo, siku hizi.

83 Lakini, loo, ni tumaini lililobarikiwa jinsi gani kwa mwamini, anayeinua mikono, kwa kuwa ukombozi wetu umekaribia. Anapona mambo haya yakitokea, ni wakati wa fahari kwa mwamini.

84 Sasa, mambo haya, huko, kuugua katika miili yetu. Je! ulipata kuuangalia mti, jinsi unavyokazana kuishi? Unataka kuishi. Na unaona mnyama fulani, jinsi ambavyo saa ya—saa ya kufa, jinsi anavyotapata. Ukimwangukia mwanadamu, kila kitu, maumbile yanaugua. Sisi, ndani yetu sisi wenyewe, tunaugua. Unaona? Tunajua kuna kasoro fulani. Tunaona,

kutokana na vifungu hivi, ya kwamba kitu fulani kimepotezwa, kwa mwanadamu na dunia pia. Viumbe vya kila namna, vimepoteza kitu fulani, kwa kuwa tunaona kutoka katika Neno hili lililovuviwa ya kwamba vinaugua kwa sababu fulani. Wewe, wewe huugui isipokuwa pawe na sababu fulani.

Kama nilivyosema juu ya wino, ni sababu fulani.

⁸⁵ Hivyo ndivyo ilivyo katika kuwaombea wagonjwa; mpaka uweze kupata sababu yake! Ninajua tiba yake, lakini sina budi kupata sababu yake. Hiyo ndiyo sababu maono ni muhimu sana na ya lazima sana; yanafunua siri za moyo, yanamwambia mtu mahali ulipofanya kosa lako, na kitu cha kufanya. Unaona? Haidhuru unywe dawa nyingi namna gani, ama utawamwagia mafuta kiasi gani vichwani mwao, ama mtu ye yote angepiga makelele juu yako kwa nguvu namna gani; kama kuna kosa fulani, yeye atakaa papo hapo. Nilisema “yeye,” huyo ni Shetani.

⁸⁶ Unaona, leo, ingawa tumeendelea sana, katika madawa, tungali hatujui cho chote juu ya mambo haya. Unasema, “Yeye ana kansa.” Vema, hilo si kitu. Hilo, hilo—hilo linataja tu jina lake. Hilo linataja jina la uganga, kansa. Hilo halina uhusiano wo wote na jinsi lilivyo. Hilo ni jina tunaloita. Tunamwita tu hilo jina, kansa. Lakini, kwa kweli, kwamba ni kitu gani, ukimchanganua, ni ibilisi.

⁸⁷ Sasa, tunasema “dhambi.” Tunaiita tu dhambi. Ivunjevunje. Dhambi ni nini? Watu wengi wanasema, “Kunywa pombe, kuzini.” La, la. Hayo ni matunda ya dhambi. Unaona? Hayo ndiyo yanayosababishwa na dhambi, unaona. Lakini dhambi yenyewe ni kutokuamini. Hapo ndipo ina— hapo ndipo inapopewa jina na kuitwa. Kama wewe ni mwamini, mambo hayo hufanyi. Lakini haidhuru unajitahidi kujifanya mtakatifu jinsi gani, na jinsi unavyokazana kuwa wa kidini; kama unafanya mambo hayo, wewe ni asiyeamini. Hilo ni la Kimaandiko.

⁸⁸ Sasa, kitu fulani kimepotea, na kinaugua. Kinajaribu kurudi, kurudia hali yake ya mwanzo.

⁸⁹ Ungemwazia mtu fulani akianguka kutoka juu ya ardhi, kuangukia chini ndani ya shimo refu mahali fulani, naye alikuwa anajitahidi, kupanda, anavuta? Wao hawana budi, kwa njia fulani, watoke katika shimo hili. Hawako katika hali yao ya mwanzo. Na, kiwenda wazimu, wanapiga makelele. Wanaparua kucha kuta, wakipiga makelele, ama wanafanya namna fulani. Wa—wanaugua kwa sababu wanataka kurudia hali yao ya mwanzoni.

⁹⁰ Hiyo ndiyo sababu mtu, aliyeshikwa na ugonjwa, kuumwa na kichwa na maumivu. Kuna wakati hawakuwa hivyo, lakini wao wanaugua. Kwa nini? Hawako na hali nzuri. Kuna kasoro fulani. Nao wanaugua, na kujaribu kurudi mahali walipokuwa wakati walipokuwa na afya.

⁹¹ Na wakati maumbile na watu, kama vile ilivyosema Biblia, “wanapougua,” inaonyesha kuna jambo fulani, ya kwamba hawako katika hali wanayopaswa kuwa. Wameanguka kutoka mahali fulani. Sasa, hatuhitaji mtu ye yote kutufasiria jambo hilo. Unaona? Kwa kuwa, bila shaka, tunajua walianguka kutoka katika Uzima wa Milele. Nao walipoteza madai yao juu ya Uzima wa Milele, kwa kule kuanguka kwa Adamu na Hawa, ambao walianguka kutoka katika Uzima wa Milele, wakaingia mautini, katika bustani ya Edeni, na wakaviingiza viumbe vyote, chini yao, kwenye mauti.

⁹² Mti haukufa kamwe, kabla ya Adamu. Mnyama asingekufa, kabla ya Adamu. Na kuna kitu kimoja tu ambacho hakiwezi kufa, na hicho ni Mungu, kwa maana Yeye ni wa Milele. Na hivyo ndivyo tu tunavyoweza kutopatikana na mauti, hatuna budi kuwa na Uzima wa Milele ndani yetu, tupate kuwa wana na binti za Mungu.

⁹³ Lakini wakati tulipokufa, kama nilivyosema katika Ujumbe asubuhi ya leo, kwa dhambi, tuliuzua haki zetu za mzaliwa wa kwanza na kuvuka shimo hili kubwa. Sasa tuko mbali mahali ambapo Mungu hawezi kutufikia, upande huu wa pili wa lile shimo kubwa. Sasa, bila shaka, wakati Adamu alipoanguka, mautini, yeye alisababisha mauti kwa viumbe vyote.

⁹⁴ Sasa, yeye alipewa hiari ya kujichagulia. Walipewa hiyo kama na sisi pia, wapate kujichagulia. Sasa, Adamu na Hawa, hapo mwanzo, kulikuwako na mti wa mema na mabaya mbele yao, na mti uo huo umewekwa mbele ya kila mtu na—na kila mmoja wetu. Unaona, Mungu hamfanyii Adamu ama Hawa... Unasema, “Vema, ni kosa lao.” La, si kosa lao sasa. Ni kosa lato. Huwezi kuliweka juu ya Adamu sasa. Huna budi kuliweka juu yako mwenyewe, kwa sababu mema na mabaya yamewekwa mbele yako. Tuko kwenye msingi ule ule kama wa Adamu na Hawa.

⁹⁵ Lakini, unaona, tunapokombolewa, hatutaki tena chaguo letu wenyewe, lakini tunataka chaguo Lake. Unaona? Unaona?

⁹⁶ Sasa, Adamu na Hawa walitaka chaguo lao wenyewe. Wao walitaka kuninii, walitaka kuona mtu unakuwaje ukiwa na hekima, kwa hiyo wakaingilia kuichunguza, na hilo likasababisha mauti.

⁹⁷ Sasa, wakati mtu anapokuwa amekwisha kukombolewa, yeye hajali tena elimu. Hayajali tena mambo ya ulimwengu, hekima ya ulimwengu. Hataki chaguo lo lote hata kidogo. Kristo amekuwa ndilo chaguo lake, na ni hayo tu basi. Amekombolewa. Hataki tena kujiongoza. Hataki mtu ye yote amshawishi aende wapi na afanye nini. Yeye hungoja tu na kutafuta chaguo la Muumba wake. Unaona? Ndipo anaenda katika jina la Muumba wake, wakati Muumba wake anapomwambia aende. Unaona?

98 Lakini mtu anayetafuta hekima, anataka kupata, “Vema, mtaa huu ni mzuri sana; lakini kule wananilipa zaidi, kwa hiyo nitaenda huko.” Unaona? Unaona, hekima.

99 Sasa, Adamu alipofanya dhambi, kwa kusikiliza kuhoji kwa mke wake badala ya kushikilia Neno la Mungu, jambo hilo ndilo lililomfanya Adamu afanye dhambi. Mke wake alihojiana na Shetani, na ndipo akampa Adamu tunda hilo, ndipo Adamu akaachilia Neno na kujiuza.

100 Alipoteza, pia, urithi wake, wakati alipopoteza ushirika wake na haki ya Uzima. Kumbuka, “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Na wakati alipopoteza Uzima wake, alipoteza pia urithi wake katika maisha, kwa sababu alikuwa na mamlaka makamilifu juu ya dunia. Yeye alikuwa mungu wa dunia hii. Mungu ni Mungu wa ulimwengu, kila mahali. Lakini mwanawe alikuwa na mamlaka juu ya dunia hii. Angeweza kunena, aliweza kutoa majina, aliweza kusema, aliweza kusimamisha maumbile, aliweza kufanya lo lote alilotaka kufanya. Unaona? Lakini, alipotenda jambo hilo, alipoteza urithi wake.

101 Sasa, Adamu aliweza kusema, “Mlima huu, hapa, na ung’oke uende pale,” na ungen’oka. Adamu angeweza kusema, “Mti huu, hapa, na ung’oke uje ukapandwe hapa,” ungefanya hivyo. Unaona? Kwa kuwa alikuwa na mamlaka kuu, na kamili, kama mungu mdogo chini ya Mungu Baba yetu, kwa maana alikuwa ni mwana wa Mungu.

102 Sasa si tungeweza kusimama hapa kidogo na kupata mahubiri mazuri kweli! Mnaona? Loo! Basi, kama ile Damu imeisafisha hiyo ikawa kama mwanzo, ni vipi sasa hivi? Unaona? Angalia yale yule Mwana wa Mungu, Adamu wa pili, aliyofanya. Mnaona? Na kasema, “Kazi nizifanyazo mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Mnaona?

103 Adamu alipoteza urithi wake, dunia. Sasa, ulitoka mkononi mwake ukaenda kwa yule aliyemwuzia, Shetani. Aliuza imani yake katika Mungu, akachukua hoja za Shetani. Kwa hiyo, Uzima wake wa Milele, haki yake kwa ule Mti wa Uzima, haki yake kwa dunia hii, ilikuwa ni mali yake, naye akapoteza kila kitu kikaenda kwenye mikono ya Shetani. Aliuota mkononi mwake akampa Shetani. Kwa hiyo, sasa, umekuwa, umerudishwa na umechafuliwa. Na uzao wa Adamu umeharibu ule urithi ambao Adamu alipaswa kuwa nao, yaani dunia hii. Hiyo ni kweli, unaona, uzao wa Adamu.

104 Nilisimama, hivi majuzi, kwenye mapambazuko huko Tucson ninakoishi. Nami nilikuwa nikizungumza na mtu fulani, huko juu kabisa mlmani, nikiangalia chini. Nikasema, “Unafikiria nini! Ya kwamba, miaka mia tatu iliyopita, Mpapago wa kale alishuka akapitia pale kwenye mkokoteni wake, pamoja na mkewe na watoto wake wameketi nyuma, akaenda pale mahali fulani na kuishi kwa amani. Hakukuwako na uzinzi, hakuna wiski,

hakuna kucheza kamari, hakukuwako na kitu cho chote kati yao. Waliishi maisha masafi. Na mbwa mwitu akashuka m-mtoni, kila usiku, kupitia hapa Tucson, akibweka. Na vichaka vya miiba na mipungate ilichanua, kingoni. Ndipo Yehova aliangalia mahali hapo na hapana budi alitabasamu. Lakini mzungu akaja huko, naye amefanya nini? Ameng'oa mipungate. Ameichafua nchi, kwa makopo ya bia na chupa za viski. Ameharibu uadilifu wa taifa hili. Njia pekee angaliweza kumwagamiza Mhindi ni kukiua chakula chake, nyati."

¹⁰⁵ Nilipokuwa nikisoma huko Tumbstone, hivi majuzi, katika je-jengo la sanaa, na kuona picha za Geronimo. Na wengi wenu huenda mkafikiri ya kwamba Geranimo alikuwa ni haini. Kwangu mimi, yeye alikuwa ni Mmarekani halisi. Alikuwa akipigania tu kile kilichokuwa cha haki, ambayo Mungu alikuwa amempa: nchi, na taifa, na mahali pa kuishi. Simlaumu. Na wakati hao askari wa kizungu walipoingia kule na, kwa kutumia nguvu, wakaitwaa nchi, na kuwaua kama kundi la nzi. Na pale ilikuwako picha ya kweli ya kituo kikuu cha matibabu cha Geronimo, ama hospitali yake. Ilikuwa tu ni mablanketi mawili ama matatu juu ya kichaka kidogo cha miiba. Na hao Wahindi halisi, wa kweli, wa Kimarekani, waliojeruhiwa, wakipigania haki zao walizopewa na Mungu. Na pale, Geronimo akimshika mtoto wake mchanga, mapajani mwake, amesimama pale akiwaangalia mashujaa wake mwenyewe, wakitokwa na damu, wakifa, bila penisilini wala cho chote kile, hana njia ya kuwasaidia; Wamarekani halisi, waliotoka kwa Mungu! Halafu ati wanamwita haini? Ninamwita muungwana.

¹⁰⁶ Kochise hangejisalimisha kamwe. Alikuwa ni mzee. Lakini Jeshi la Marekani, wakajiandaa wote kule ndani, nao walitoka wakaenda kule na wangewaua nyati. Walifanya mashambulizi kule, ndipo Sharpe akagundua bunduki ya nyati, nao wakatoka wakaenda kule na kusema, "Loo, nilikuwa na siku nzuri leo," wakiwapiga risasi, kutoka upande mmoja wa bo- bogi, ama behewa la gari la abiria. Wanasema, "Niliua arobaini leo." Nyati arobaini, ambao wangaliweza kudumisha kabila zima la Wahindi, miaka miwili ama zaidi. Walifanya nini nao? Waliwaacha wamezagaa huko nyikani. Mizoga yao iliyooza ikapasuka katika nchi, na kuifanya nchi inuke, mbwa mwitu wakaila.

¹⁰⁷ Wahindi walipoua nyati, kulikuwako na sherehe ya kidini. Alichukua kwato zake, akazihifadhi apate kutengeneza vikaango. Wakala nyama yake, hata matumbo yake. Walichukua nyama yake yote na kuining'iniza na kuikausha. Ngozi yake ilikaushwa, nao wakatengeneza mavazi na mahema. Hakukuwa na kitu cho chote. . .

¹⁰⁸ Lakini, wakati mzungu alipoingia, mzungu ndiye haini. Yeye ndiye mhuni. Naye alikuja na kuwaua hao nyati, na kuwaua hao Wahindi kwa njaa.

109 Mtu ye yote timamu angepigania haki zake alizopewa na Mungu. Ni waa kwenye bendera ya Marekani, yale waliyowatendea Wahindi wa Kimarekani. Hata hivyo, yote ilikuwa ni yake.

110 Ungewaziaje kama Japa-. . . Japani, ama—ama ninii fulani, Urusi ingekuja, na kusema, “Ondokeni hapa! Ondokeni hapa,” na—na kutufanyia sisi pamoja na watoto wetu jinsi tulivyowafanyia hao Wahindi? Lakini, kumbukeni, tumepanda, na sasa tutavuna. Hiyo ndiyo sheria ya Mungu, mwajua. Kuna wakati wa kupanda, halafu tena wakati wa kuvuna. Nafikiri jambo hilo ni baya sana. Naam, bwana.

111 Sasa ni jambo gani lilitukia? Uzao wa Adamu uliochafuka umeichafua na kuiangamiza nchi kabisa. Unajua ya kwamba Biblia inasema jambo hilo? Na kwa sababu amefanya jambo hili, uzao wa Adamu uliochafuka, Mungu atawaangamiza. Mnataka kusoma hilo? Hebu na tuone. Nimeliandika hapa. Fungueni Ufunuo, sura ya 11, nasi tutaona. Fungueni katika Ufunuo, sura ya 11, nasi tutaona yale Mungu aliyosema juu ya hao wanaoiharibu nchi. Sura ya 11, na hebu tuchukue fungu la 18, ninaamini ndiyo, 11:18. Hii hapa.

Na mataifa walikasirika, na hasira yako nayo ikaja (Sasa angalia hasira ya Mungu), na wakati ukaja wa kuhukumiwa waliokufa, na wa kuwapa thawabu yao watumwa wako manabii na watakatifu, na hao walichao jina lako, wadogo kwa wakubwa pia, na wa kuwaharibu hao waiharibuo—waiharibuo nchi.

112 Watafanya nini? Watavuna walichopanda. Hakika. Unapooona dhambi imejaa mitaani! Ni wangapi, katika usiku huu wa Jumapili, ni uzinzi mngapi utafanywa katika jiji hili usiku wa leo? Ni wanawake wangapi watakaovunja nadhiri yake ya ndoa, katika shimo hili dogo hapa ardhini, linaloitwa Jeffersonville? Unafikiri ni kutoa mimba kungapi kunakoandikishwa Chicago, katika siku thelathini? Ni kati ya elfu ishirini na tano na elfu thelathini kwa mwezi, mbali na zile ambazo hazikuripotiwa. Ni kiasi gani cha wiski kinanywewa katika jiji la Chicago? Unafikiri ni kitu gani kinachotendeka huko Los Angeles katika usiku mmoja? Ni mara ngapi Jina la Bwana limetajwa bure, katika jiji la Jeffersonville leo? Je! bora siku hizi, ama ulikuwa na bora wakati George Rogers Clark aliposhuka kuja kwa chelezo? Mnaona, tumeichafua dunia kabisa kwa uchafu wetu, na Mungu atawaangamiza hao wanaoangamiza nchi. Mungu alisema hivyo.

113 Daima nilifikiri kulikuwako na kitu fulani ndani yangu, kinachopenda kupanda milima na kuangalia jinsi Mungu alivyoiumba.

114 Ninachukia, Florida, ambako wana hiyo mitende isiyoyasili ya hapo. Na, loo, jamani, afadhali niwaone mamba

wakitikisa mkia wake, huko ndani mwituni, kuliko kuona mambo hayo yote kule ya bandia na upuuzi wanaofanya huko Hollywood, na urembo wote wa kudanganya macho, na kundi la walevi. Na, loo, jamani, ninawazia tu, “Siku moja! Siku moja!” Naam.

115 Lakini, kumbukeni, Biblia imetwambia, katika Mathayo sura ya 5, ya kwamba, “Wenye upole watairithi nchi.” Hiyo ni kweli. “Wenye upole na wanyenyekevu watairithi nchi.” Yesu alisema, “Heri wenye upole,” watu wanyenyekevu wasiojaribu kuwa kitu fulani kikubwa mno, “watairithi nchi.” Yesu alisema hivyo. Naam. Sasa wao waliichafua, naye Mungu atawaangamiza; lakini wenye upole watairithi nchi, ikiisha kusafishwa.

116 Sasa, loo, jamani! Sasa, ile hati-miliki iliyopotezwa sasa iko mikononi mwa Mwenyewe wa asili, Mwenyezi Mungu. Hati-miliki ya dunia, na ya Uzima wa Milele, wakati Adamu alipoipoteza; ndipo mikono michafu ya Shetani haikuweza kuichukua, kwa hiyo ilimrudia Mwenyewe wa asili, Mungu Mwenyewe. Tutaona jambo hilo, punde si punde tu. Huyo hapo ameketi kwenye Kiti cha Enzi, akiwa nayo mkononi Mwake, ile hati-miliki. [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.] Loo, hilo linanifanya kujisikia wa kidini. Hati ya kumiliki ya Uzima wa Milele, hati-miliki ya siri ya Uzima wa Milele, wakati Adamu alipoipoteza kwa ajili ya hekima, badala ya imani, ilirudi kwenye mikono ya Mwenyewe, Mwenyezi Mungu. Ni jambo kuu jinsi gani!

117 Vema, kungojea. Inafanya nini? Katika mikono ya Mungu, ikingojea madai ya ukombozi. Yeye alifanya njia ya ukombozi, alifanya njia ya kurudi, na siku moja Mkombozi huyo atairudisha. Unaona mahali tunakoelekea sasa? Tutamwangalia Mtu huyu anayeketi kwenye Kiti cha Enzi. Vema, akingojea madai ya ukombozi, ukombozi wa hiyo.

118 Kitabu hiki cha Ukombozi ni nini, hii hati-miliki, hati-miliki ya kuwazika?” “Unasema, ‘ati ya kuwazika?’” Maana ya siri ni nini? Inamaanisha imefuatiliwa kule nyuma kabisa mpaka mwanzo wake. Kama lile—kama lile tone dogo la wino asubuhi ya leo, wakati lilipodondokea kwenye kile kitakasaji, lilirudi moja kwa moja huko nyuma kabisa. Na wakati dhambi imekwisha kutubiwa na kuangukia kwenye Damu ya Yesu Kristo, loo, jamani, inatoa siri, moja kwa moja inarudi kwa Muumba tena. Unakuwa mwana wa Mungu. Hati-miliki ya kuwazika iko katika mikono ya Mwenyezi. Loo, jamani!

119 Ukombozi wake unamaanisha umilikaji halali wa yote yaliyopotezwa na Adamu na Hawa. Loo, jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja.] Hilo linapaswa kumfanyia nini Mkristo aliyezaliwa mara ya pili! Umilikaji wake wa halali wa hiyo hati-miliki ya kuwazika, hati-miliki

ya Uzima wa Milele, inamaanisha ya kwamba wewe una kila kitu ambacho Adamu na Hawa walikipoteza. Whiu! Vipi kuhusu jambo hilo, ndugu? Kuipata hati hiyo!

¹²⁰ Adamu hangeweza kutimiza masharti ya ukombozi. Baada ya yeye kuona kwamba aliipoteza, alikuwa ametenda dhambi na alikuwa amejitenga na Mungu, alikuwa upande *huu* wa lile shimo kubwa, kwa hiyo hangeweza kuikomboa. Yeye hangeweza kufanya hivyo kamwe, maana a-alihitaji ukombozi, yeye mwenyewe, kwa hiyo hangeweza kufanya jambo hilo.

¹²¹ Lakini ile sheria ilihitaji Mkombozi aliye Jamaa ya Karibu. Sheria ya Mungu ilihitaji Mkombozi aliye wa Jamaa ya Karibu. Ukitaka kuandika hilo, “Mkombozi aliye wa Jamaa ya Karibu,” utalipata katika Mambo ya Walawi 25.

¹²² Hatutapata wakati wa kuchunguza jambo hili kindani sana, maana, mwajua, kila—kila kifungu kingechukua u—usiku mzima. Mnaona?

¹²³ Lakini sheria ya Mungu ilipokea kibadala. Sasa, vipi kama Mungu hakuwa amejitolea kutoa kibadala? Lakini upendo ulimshurutisha kufanya jambo hilo. Kwamba, mwanadamu hakuwa na njia ya kurudia, na hakuna njia kwake ya kurudi. Alikuwa amepotea. Lakini neema ya Mungu ilimtoa huyu Mkombozi aliye wa Jamaa ya Karibu katika Utu wa Yesu Kristo. Sheria ilihitaji jambo hilo. Neema ikatimiza masharti yake. Loo, neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu! Sheria ya Mungu ilihitaji kibadala kisicho na hatia.

¹²⁴ Na ni nani ambaye hakuwa na hatia? Kila mtu alikuwa amezaliwa kwa kujuana kimwili, kwa kujuana kimwili, kila mmoja. Na yule pekee asiyekuwa hivyo, alikuwa amepoteza haki za Uzima wa Milele na ya yeye kuwa mfalme duniani.

¹²⁵ Loo, ninapowazia Andiko hilo, “Kwa kuwa umetukomboa kuturudisha kwa Mungu, na tupate kutawala na kuwa wafalme na makuhani juu ya nchi.” Loo, jamani! Ni nini? Mkombozi aliye wa Jamaa ya Karibu! Loo, ni habari ya namna gani tungeisimulia hapa!

¹²⁶ Angalia, sheria ilihitaji Mkombozi aliye wa Jamaa ya Karibu ili kukomboa kitu kilichopotea. Neema ilitimiza sharti hili katika Utu wa Yesu Kristo. Jamaa wa Karibu hana budi kuzaliwa kwa jamii ya binadamu.

¹²⁷ Sasa, tungewezaje kuwa huyo, wakati kila mtu aliyezaliwa hana budi kunini. . . Na mtu ye yote asiyeweza kuona lilikuwa ni tendo la kujuana kimwili pale, vema, yeye ni kipofu kabisa, unaona, maana kila mtu aliyepata kuzaliwa alizaliwa na mwanamke.

¹²⁸ Na Mungu alihitaji Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu, naye hana budi kuwa ni mwanadamu. Loo, jamani! Mtafanya nini sasa? Sheria ilitaka Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu.

129 Sasa, Yeye asingeweza kuchukua Malaika. Ilibidi amchukue mwanadamu, maana sisi si wa ukoo wa Malaika. Sisi ni ndugu sisi kwa sisi. Malaika hakuanguka kamwe. Yeye ni kiumbe cha namna nyingine, ana mwili tofauti. Yeye hakufanya dhambi wala cho chote kile. Yeye ni tofauti.

Lakini sheria ilitaka Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu.

130 Na kila mtu duniani alizaliwa kwa kujuana kimwili. Sasa, je! hamwoni, hapo ndipo hilo lilipochimbuka. Hapo ndipo dhambi ilipoanzia. Kwa hiyo unaona mahali jambo hilo lilipo sasa? Huyu hapo anakuja, uzao wenu wa nyoka, unapoingia. Unaona?

131 Sasa, angalia, alihitaji Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu. Na huyo Mkombozi, Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu, hana budi kuzaliwa na jamii ya binadamu. Hapa, hiyo inatuacha mahali pa hatari. Lakini hebu niwapigie Baragumu. Ule uzazi wa kibikira ulimleta yule—yule mzao. Amina. Uzazi wa kibikira ulimzaa Mkombozi aliye Jamaa yetu wa Karibu. Si mwingine bali ni Mwenyezi Mungu aliyefanyika Imanueli, mmoja wetu. Imanueli! Yule “Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu” alipatikana. Unaona jinsi Mungu anavyotoa masharti fulani, na hakuna jambo tunaloweza kufanya. Lakini basi neema inaingia na kuizidi hiyo sheria, na kuleta ule uzao. Amina! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.]

132 Loo, mtakapofika Nyumbani! Nitakapopata kibanda changu kidogo kule; ambacho Ndugu Neville anaimba habari zake. Wakati ninyi nyote mtakaposikia kitu fulani kule chini, asubuhi moja, kikiimba, “Neema ya ajabu, jinsi sauti yake ilivyo tamu, iliyomwoko maskini kama mimi!” Mseme, “Mungu asifiwe! Maskini Ndugu Branham alifaulu. Huyu hapo, mnaona.” Naam. Loo!

Neema ndiyo iliyofundisha moyo wangu
kuhofu,

Neema ndiyo iliyoniondolea hofu zangu;

Jinsi neema hiyo ilivyoonekana kuwa ya
thamani

Ile saa niliyoamini mara ya kwanza!

133 Ngoja mpaka tutakapofikia jambo hilo, hivi punde tu! Loo, jamani! Sasa angalia. Kile Kitabu. . .

134 Kitabu cha Ruthu kinatoa picha nzuri ya jambo hili, jinsi Boazi. . . Na Naomi walivyokuwa wamepoteza shamba. Ninyi, mnajua. Mlinisikia nikihubiri juu ya jambo hilo, sivyo? Inueni mikono yenu kama mlinisikia nikihubiri juu ya jambo hilo. Kwa hiyo, mnafahamu, mnaona. Ilimbidi Boazi awe mkombozi. Naye ndiye tu ambaye angaliweza kuwa mkombozi. Ilimbidi awe jamaa, jamaa wa karibu. Na, katika kumkomboa Naomi, alimpata Ruthu. Huyu alikuwa ni Yesu, Boazi akiwa ni mfano wa Kristo. Na alipowakomboa Israeli, alimpata Bibi-arusi

Mmataifa. Kwa hiyo basi, mnaona, ni zuri mno! Tunalo katika kanda, nina hakika, hapa mahali fulani, mkitaka kulipata.

¹³⁵ Sasa angalia, sasa, hana budi kuwa Jamaa wa Karibu. Kwa hiyo, unaona, Malaika hangeweza kufanya jambo hilo. Mwanadamu asingeweza kufanya jambo hilo; hana budi awe mwanadamu, lakini hawezi kuzaliwa na mwanamke, tendo la kujuana kimwili. Kwa hiyo, uzazi wa kibikira, Roho Mtakatifu alimtia uvuli Mariamu. Kwa hiyo, Yesu hakuwa Myahudi. Yesu hakuwa Mmataifa. Yesu alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Damu yake haikutokana na tendo lo lote la kujuana kimwili. Alikuwa Damu takatifu, iliyoumbwa na Mungu. Nasi hatuokolewi kwa damu ya Kiyahudi, wala hatuokolewi na damu ya Mmataifa. "Tunaokolewa na Damu ya Mungu." Hiyo ni kulingana na Biblia. Inasema hivyo. "Tunaokolewa na . . ."

¹³⁶ Kwa hiyo, unaona, Yesu alikuwa ni Mungu. Hakuwa Nafsi ya tatu, Nafsi ya Nne, Nafsi ya pili. Alikuwa ndiye ile Nafsi Yenyewe. Alikuwa Mungu, unaona. Alikuwa Mungu, Imanueli. Mungu alishuka kutoka katika Utukufu Wake, akajifunua Mwenyewe. Ninapenda ile hadithi, ya Booth-Clibborn, ule wimbo mashuhuri, mzuri.

Alishuka kutoka katika Utukufu Wake,
hadithi iliyo hai daima,
Mungu wangu na Mwokozi wangu alikuja, na
Jina Lake lilikuwa ni Yesu.
Alizaliwa katika hori, akiwa mgeni kwa walio
Wake,
Mtu wa huzuni, machozi na uchungu. Loo!

Ni kujidhili kwa namna gani, kukituletea
ukombozi;
Ambapo katika usiku wa manane,
hapakuonekana hata na tumaini moja dogo
kabisa;
Mungu, wa thamani, mwenye upendo, aliweka
kando fahari Zake,
Akainama apate kuibembeleza na kuiokoa
nafsi yangu.

Ee jinsi ninavyompenda! Jinsi
ninavyomwabudu!
Pumzi yangu, nuru yangu ya jua, yote katika
yote kwangu!
Yule Mkombozi mkuu alifanyika Mwokozi
wangu,
Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi
wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani
Yake.

137 Huyu ndiye aliyetimiza lile sharti. Neema ilileta Utu wa Yesu Kristo. Nasi tunaona, Kitabu hiki sasa...Mungu alitandaza hema Yake, iliyotoka kwa Mungu, akafanyika mwanadamu. Alibadili hali Yake, kutoka kuwa Mwenyezi, akawa mwanadamu; kuchukua umbo la mwanadamu, apate kufa, ili amkomboe mwanadamu. Ngoja mpaka tutakapomwona, wakati hakuna mtu ye yote anayestahili." Unaona? Vema.

138 Katika Biblia, katika Kitabu cha Ruthu, unapokisoma, utaona kwamba, mtu kama huyo aliitwa "goel," g-o-e-l. Aliitwa goel, ama, alikuwa ni mtu fulani ambaye angeweza kutimiza masharti hayo. Na goel hana budi kuwa anaweza kufanya jambo hilo, hana budi kuwa tayari kufanya jambo hilo, na hana budi kuwa jamaa, jamaa aliye wa karibu, ili kufanya jambo hilo.

139 Na Mungu, yule Muumba, wa Roho, akafanyika jamaa yetu wa karibu hapo Yeye alipofanyika mtu, kusudi kwamba aweze kujitwika dhambi yetu, na kulipia gharama, na kutukomboa kurudi kwa Mungu tena. Hivyo ndivyo ilivyo. Huyu hapo yule Mkombozi.

140 Kristo ametukomboa sasa. Sasa sisi tumekombolewa. Lakini bado hajadai mali yake. Sasa, unaweza kutokukubaliana na jambo hilo, lakini ngoja tu kidogo, unaona. Tutaona. Unaona? Hajaidai. Unaona? Kama alikitwaa kile Kitabu cha Ukombozi, kila kitu ambacho Adamu alikuwa nacho na kila kitu ambacho alipoteza, Kristo anakikomboa na kukirudisha. Naye tayari ametukomboa. Lakini bado hajachukua mamlaka; hawezi mpaka wakati ulioamriwa. Na ndipo utakuja ufufuo, na halafu dunia itafanywa upya tena. Na ndipo atamiliki, mali Yake aliyopata hapo alipotukomboa sisi, lakini atafanya hivyo katika wakati ulioamriwa. Loo, jamani!

141 Jambo hili limeelezwa katika Kitabu hiki cha Mihuri Saba tunachonena habari zake sasa. Vema. Kitabu cha Ukombozi, yote yameelezwa hapa ndani. Yote yale ambayo Kristo atafanya wakati wa mwisho yatafunuliwa kwetu juma hili, katika ile Mihuri Saba, kama Mungu ataturuhusu. Unaona? Vema. Yatafunuliwa. Na kufunuliwa, wakati Mihuri hii inapovunjwa na kufunguliwa kwetu, ndipo tunaweza kuona mpango huu mkubwa wa ukombozi ulivyo, na ni lini na ni vipi utafanyika. Yote yamefichwa katika Kitabu hiki cha siri hapa. Kimetiwa muhuri, kimefungwa kwa Mihuri Saba, na kwa hiyo Mwana-Kondoo Ndiye pekee Ambaye anaweza kuivunja.

142 Sasa...[Ndugu Branham anakatizwa na kitu fulani—Mh.] Samahani. Tunatambua... .

143 Sasa, kama mngetaka kuyachunguza Maandiko, mnaweza kufungua katika Yeremia na kuchunguza hapo. Wakati alipokuwa—wakati a—alipokuwa akienda utumwani mwa ile nchi, mwajua, a—alimnunulia mjomba wake...Mwana wa

mjomba wake alikuwa na mali fu—fulani, naye akapitia jambo hilo, kutia muhuri. Na kama tungelichukua lote. . . Tulipata jambo hilo pia katika zile *Nyakati Saba za Kanisa*, hiyo mihuri na kadhalika, mle ndani.

¹⁴⁴ Unaona, mhuri, katika Agano la Kale, ulikuwa kama kitu kilichovingirishwa, namna *hii*. [Ndugu Branham sasa anatomia makaratasi kuonyesha kule kufingirishwa, kutiwa muhuri, na kufunguliwa kwa gombo—Mh.] Na *hapa* ilikuwepo siri fulani, na siri hii ilikuwa imefichwa. Vema, ilikuwa imetiwa mhuri na kuwekwa hapa, dai la *fulani*. Ndipo, hiyo siri nyingine ilikuwa imefingirishwa kwenye kile huu urithi mwingine ulichokuwa, na kuambatanisha hapa upande *huu*, lile—lile—lile dai la *fulani*. Na ikaendelea moja kwa moja mpaka ikafanya gombo, kwa sababu watu hawakuwa na vitabu kama *hiki* wakati huo. Kilikuwa ni kitu kilichofingirishwa, (ni wangapi wanaojua jambo hilo?) kilichoitwa gombo. Vema, gombo lililotiwa muhuri, ungeweza kuvunja mmoja *hapa*, kwamba siri ya hii ilikuwa ni nini, na kuuchana ili kuufungua, na ungeweza kuona dai hilo lilikuwa ni nini. Kisha uvunje ule mwingine, na unaweza kuona dai hilo lilikuwa ni nini.

¹⁴⁵ Na kitu hicho chote Hapa ni ile Mihuri Saba, iliyo na siri za Mungu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu zimetiwa muhuri zote Mle ndani, na kufunuliwa na Mihuri saba mbalimbali, ambapo, Mungu akipenda, aturuhusu tufunue Mihuri hii na kukichunguza Kitabu hiki na kuona kinahusu nini. Mnaona? Loo, ninatumaini tutakuwa na wakati mzuri sana! Ile siri ya ukombozi imetiwa muhuri humo mpaka. . . Kitabu hiki hakingeweza kuvunjwa mpaka kwenye ule Ujumbe wa Malaika wa mwisho.

¹⁴⁶ Lile gombo liko pale. Tulijua lilikuwapo. Tunajua ya kwamba ilikuwa ni ukombozi. Tuliadini ilikuwa ni ukombozi. Yereimia alisema, “Gombo hili halina budi kuwekwa. . .” Unaposoma pale, atasema. Hana budi kuwekwa katika chombo cha udongo. Unaona? Loo, ni jambo zuri jinsi gani pale ningaliweza kunena habari zake, kwa muda kidogo. Gombo hili liliwekwa katika chombo cha udongo, chombo ambacho wakati mmoja kilifanyika mwili (utukufu!), kikafa, kikafufuka tena, na kuwekwa katika chombo cha udongo mpaka wakati wa kununuliwa. Loo, jamani! Inafurahisha! Naam.

¹⁴⁷ Sasa, Jumbe hizi zote zimewekwa mpaka, chombo hiki cha udongo, mpaka saa ya wakati ulioamriwa na Mungu, wakati wa yule mjumbe wa mwisho duniani. Na yote yale ambayo watu hawa waliyokuwa wamefikiria, na kusema, “Ninajua lipo. Ninaadini lipo.” Nao wakalipigania, na kulihubiri na kusababisha mambo mbalimbali. Kwa imani waliadini Hilo. Lakini sasa litaletwa kwetu katika ufunuo, na kutoka katika mkono wa Mungu kwa kuthibitishwa. Mungu alisema jambo hilo. Aliliahidi.

148 Sasa, sasa hebu na tuone. Tulikuwa, tulikuwa wapi? Hebu na twende kwenye kifungu cha 2 sasa. Huo ni muda mrefu sana kwa kifungu cha 1, lakini hebu—hebu—hebu na tuchukue kifungu cha 2. Sasa, labda hatutakaa muda mrefu namna hiyo katika hiki kimoja kinachofuata.

Nami nikaona malaika mwenye nguvu akihubiri kwa sauti kuu, Nnani astahiliye kukifungua . . . kitabu, na kuzivunja muhuri zake?

149 Sasa, kumbukeni. Hebu na tusome kifungu cha kwanza tena, kusudi tulipate kwa pamoja.

. . . nikaona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi . . .

150 Mungu! Huyu ni nani? Yule wa asili kabisa mwenye kukishika kile Kitabu cha Uzima. Yeye anakishikilia. Mungu anakishikilia. Wakati Adamu alipokipoteza, kilimrudia Mwenyewe wa asili. Ni mali Yake.

Kisha Yohana (katika lile ono) akaangalia na kuona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi ki—kitabu kilichoandikwa ndani na nyuma, kimetiwa muhuri saba.

151 Unaona, ndani! Sasa, tutakapoanza kuivunja Mihuri hii, mtaona, zinarudi moja kwa moja nyuma kwenye Maandiko, kule nyuma kabisa, kwa kila moja ya ile Mihuri. Jambo lote zima, pamoja, siri yote, iko papa hapa katika Mihuri hii. Unaona? Kila siri ya Biblia iko katika Mihuri hii. [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara tano—Mh.] Na Mihuri hii haiwezi kuvunjwa mpaka wakati huo. Nitathibitisha jambo hilo hapa, punde si punde.

152 Angalia. Sasa, kile Kitabu, kumbukeni, kimetiwa muhuri. Huu hapa mmoja, Huu hapa, muhuri *huu*. Halafu Ule mwingine umekunjwa, Muhuri. Mwingine umekunjwa, Muhuri. Ni Kitabu cha Ukombozi. Na kitu hicho chote, pamoja, kinafanyiza kile Kitabu, nacho kimetiwa Mihuri Saba. Na, halafu, iko upande wa nyuma, ni kwa sababu zimekunjwa. Siri ya ule Muhuri iko upande wa ndani. Na inasema tu, “Mpanda farasi mweupe,” ama, “Mpanda farasi mweusi,” na kadhalika, upande wa nje. Lakini ile siri ya Kitabu hicho chote imo kwenye hiyo Mihuri, kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo. Ule mpango mzima wa ukombozi umefunuliwa katika Mihuri hii Saba. Loo, ni wakati muhimu. Mungu atusaidie kulipata! Unaona?

153 Sasa, “Na malaika mwenye nguvu . . .” Sasa kifungu cha 2.

. . . malaika mwenye nguvu kwa sauti kuu, akitangaza, Nnani astahiliye . . . (Astahiliye kwa kitu gani?) Nnani astahiliye kukitwaa kitabu hicho, . . .

154 Sasa tunaona. Kile Kitabu kiko wapi sasa? Kwa Mwenyewe wa asili, kwa maana kimepotezwa na mwana, mwana wa kwanza

wa Mungu, katika jamii ya binadamu. Na wakati alipozipoteza haki zake, kumsikiliza Shetani, aliacha . . . Alifanya nini? Alikubali hekima ya Shetani badala ya Neno la Mungu. Sasa, hebu tusimame hapa kidogo! Wana wa Mungu watachukua wazo la seminari juu ya jambo Hilo, badala ya Neno la Mungu. Unaona, ni jambo lile lile alilofanya Adamu, akazipoteza haki zake. Na wakati alipofanya jambo hilo, zilirudi moja kwa moja. Hivi hamwezi kuona mahali nyakati hizo zilipokuwa? Unaona? Kilirudi moja kwa moja kwa mwenyewe wa asili.

¹⁵⁵ Naye Yohana, katika Roho, akisimama juu hapa Mbinguni. Yeye ndiyo kwanza ainuliwe juu sasa, kutoka katika zile nyakati za kanisa, unaona, akazia nyakati za kanisa. Na ndipo akatwaliwa juu, katika mlango wa 4. Yeye akasema, “Panda hata huku. Nitakuonyesha mambo yatakayokuja.”

¹⁵⁶ Naye akaona Mmoja aliyeketi kwenye kile Kiti cha Enzi, ameshika Kitabu hiki mkononi Mwake, katika mkono Wake wa kuume. Wazia jambo hilo, sasa. Na, halafu, katika Kitabu hiki kulikuwako na hati-miliki ya ukombozi, nayo ilikuwa imetiwa Muhuri kwa Mihuri Saba.

¹⁵⁷ Ndipo akatokea Malaika, Malaika mwenye nguvu, akitangaza kwa sauti kuu, “N’nani alistahili kukifungua hicho Kitabu; kukitwaa hicho Kitabu? N’nani aliyeweza kuifungua ile Mihuri? N’nani aliyeweza kukifungua Kitabu hiki?” Unaona, yule Malaika aliuliza swali hilo. Yohana aliona jambo hilo. Ndipo akasema, “Sasa, n’nani astahiliye? Na aninii . . .” Loo, jamani! Labda ninasikia tu jambo hili, namna hii. “Lakini hebu Yeye,” kasema yule Malaika, “hebu Yeye . . .” *Hiki* hapa kile Kitabu cha Ukombozi! *Huu* hapa ule mpango wa ukombozi! *Hii* hapa njia pekee utakayokombolewa kwayo, kwa maana *hii* hapa ndiyo hati-miliki ya ukombozi wa mbingu zote na nchi! “Na aje mbele, kama akitaka.” Loo, jamani! “Sasa na anene, la sivyo anyamaze milele. Na aje mbele akakidai Kitabu hiki. Ni nani astahiliye kufanya jambo hilo?”

¹⁵⁸ Ndipo Yohana akasema:

Hapakuwapo na *mtu mbinguni* aliyestahili; hapakuwa na mtu *juu ya nchi* aliyestahili; hakuna mtu chini ya *nchi*, aliyepata kuishi na kufa, aliyeonekana anastahili. Hakuna mtu aliyeonekana anastahili.

¹⁵⁹ Wito wa yule Malaika ulikuwa wito wa Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu kutokea. Mungu alisema, “Nina sheria; Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu anaweza—anaweza kuwa kibadala Mkombozi huyo aliye Jamaa wa Karibu yuko wapi? N’nani anayeweza kukitwaa?”

¹⁶⁰ Nacho kilitoka kwa Adamu, kote kote kupitia kwa mitume wote, na manabii, na cho chote kile, wala hakuna aliyepatikana. Sasa, na hilo je? “Hakuna mtu Mbinguni, hakuna mtu duniani, hakuna mtu aliyepata kuishi.” Eliya alikuwa amesimama

pale. Musa alikuwa amesimama pale. Mitume wote walikuwa wamesimama pale, ama—ama wote waliokuwa wamekufa; watakatifu wote, Ayubu, wale wenye hekima. Kila mmoja alikuwa amesimama pale, wala hakuna mtu aliyestahili hata kukiangalia kile Kitabu, licha ya kukitwaa na kuivunja ile Mihuri.

¹⁶¹ Sasa akina papa na hawa wengine wote wanaingilia wapi? Askofu wenu yuko wapi? Kustahili kwetu kuko wapi? Sisi si kitu. Hiyo ni kweli.

¹⁶² Yeye alitaka Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu ajitokeze mbele, kama angeweza. Lakini Yohana alisema, “Hakuna mtu aliyestahili.”

¹⁶³ Si kwamba hakukuwako na watu waliostahili pale, sasa, kama vile Malaika; kama vile, kwa mfano, tungesema, Gabrieli, ama Mikaeli. Lakini, kumbukeni, ilipaswa kuwa ni Mtu aliye Jamaa wa Karibu. Kumbukeni, Yohana alisema hapa, “Wala hakuna m-t-u,” si Malaika, si Kerubi. Wao hawakuwa wametenda dhambi, lakini Hao walikuwa wa jamii nyingine. Hawajaanguka kamwe.

¹⁶⁴ Lakini huyu alipaswa kuwa Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu. “Hakuna mtu,” maana hapakuwepo na mmoja wao aliyekuwa amekombolewa. “Hakuna mtu aliyestahili kukiangalia.” Loo, la! Jamani, jamani! Kwa hiyo, ilitakiwa Jamaa wa Karibu wa kibinadamu. Naye akamwulizia huyo, wala hakupatikana, mahali po pote. Hapakuwapo na mtu ye yote. Hakuna cha askofu, hakuna cha askofu mkuu, hakuna cha kasisi, hakuna cha jamii ya makasisi, hakuna kitu kilichokuwa hata... hawakuwa hata na utakatifu wa kutosha hata kukiangalia Kitabu hicho. Whiu! Jamani, jamani! Hilo ni kali kweli kweli, lakini hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Ninanukuu tu yale aliyosema Yohana.

Biblia ilisema ya kwamba Yohana “alilia.”

¹⁶⁵ Si kama vile baadhi ya watu walivyofundisha jambo hilo. Nilikuwa nikimsikia mtu fulani akifundisha jambo hili wakati mmoja, kasema, “Yohana alilia kwa sababu alijiona yeye mwenyewe hakustahili.” Loo! Mtu ye yote chini ya Roho Mtakatifu angejua tofauti na hivyo, unaona; chini ya upako wa Mungu, angejua tofauti na hivyo.

¹⁶⁶ Lakini, Yohana “alilia.” Hili hapa ndilo ninafikiri lilikuwa sababu ya kulia kwake. Kwa sababu, kama hakuna mtu aliyestahili na angeweza kukifungua Kitabu hiki cha Ukombozi, viumbe vyote vilikuwa vimepotea.

¹⁶⁷ *Hiki* hapa hicho Kitabu, *hii* hapa ile hati-miliki, nayo itatolewa kwa Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu ambaye anaweza kustahili. Hiyo ndiyo sheria ya Mungu Mwenyewe, na Yeye hawezi kuchafua sheria Yake, hawezi kukana sheria Yake, hasa. Unaona? Mungu alihitaji Mkombozi aliye Jamaa

wa Karibu aliyestahili, Ambaye aliweza kufanya jambo hilo, Ambaye alikuwa na mali ya kufanyia jambo hilo.

168 Ndipo yule Malaika akasema, “Sasa hebu yule Mkombozi wa Jamaa wa karibu na akaribie.”

169 Na Yohana akaangalia. Na akaangalia kila mahali duniani. Akaangalia chini ya dunia. Na hapakuwapo na mtu. Viumbe na cho chote kile vilikuwa vimepotea. Bila shaka, Yohana alilia. Kila kitu kilikuwa kimepotea.

170 Kulia kwake hakukudumu ila dakika moja tu, hata hivyo. Ndipo akasimama mmoja wa wale wazee, kasema, “Usilie, Yohana.” Loo, jamani! Kulia kwake hakukudumu ila dakika moja tu.

171 Yohana akawazia, “Loo, jamani, yuko wapi Mtu huyo? Manabii wako pale wamesimama; walizaliwa kama nilivyozaliwa mimi. Wenye hekima wako pale wamesimama. Wale pale wamesimama . . . Loo, je! hakuna mtu hapa?”

172 “Ninataka Mtu anayeweza kufanya jambo hilo. Ninataka Mtu anayeweza kukomboa.”

173 Wala hakupatikana, kwa hiyo Yohana akalia. Loo, kila kitu kilikuwa kimepotea; naye akalia kwa uchungu. Na a-alikuwa na huzuni, maana kila kitu, viumbe vyote, kila kitu kilikuwa kimepotea, kama wasingeweza kumpata mtu. Utukufu kwa Mungu! Kama hawangeweza kumpata mtu anayeweza kutimiza yale masharti, kungeninii . . . kila mwanadamu, na ulimwengu wote na viumbe, vimepotea. Loo, kila kitu kilikuwa kimeanguka. Zile—zile—zile haki za ukombozi, zile haki za—za Uzima wa Milele, ile Nuru, haki hizi zote zilikuwa zimepotezwa, wala hapakuwapo na mtu ye yote ambaye angeliweza kulipia ile gharama. Ndipo Yohana anaanza kulia, maana hakuna mtu aliyestahili, wala hakuna mtu angaliweza hata kukiangalia kile Kitabu. Loo, ilitakiwa mwanadamu. Yohana akalia, kwa sababu hakuna mtu angaliweza kufanya jambo hilo, na kila kitu kilikuwa kimepotea.

174 Ndipo kukatokea sauti kutoka mmoja wa wale wazee, aliyekuwa amesimama kati ya wale Wenye Uhai wanne na jeshi hilo lote la Mbinguni, kasema, “Usilie, Yohana.” Loo, jamani!

175 [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.] Neema ya Mungu!

176 “Usife moyo, Yohana. Usilie. Kwa kuwa Simba wa kabila ya Yuda, aliye Shina na Mzao kutoka kwa Daudi, ameshinda.”

177 *Kushinda* maana yake ni “kushindana kwa nguvu, na kutiisha.” Loo, jamani! Bustani ya Gethsemane, wakati Damu ilipotiririka kutoka katika uso Wake, Yeye alikuwa akitiisha. Unaona? Whiu! Unaona?

178 “Yule Simba, na aliye Shina la Daudi, ameshindana kwa nguvu, ametiisha.”

179 Kama vile Yakobo, akiwa mdanganyifu. Na wakati alipokutana na yule Malaika, alishikilia. Naye Malaika akajaribu kujinasua. Akasema, “Ya—yakini sitakuruhusu uondoke.” Alishikilia hata akapata alichotaka. Nalo jina lake likabadilishwa, kutoka *mdanganyifu*, ambalo maana yake ni “mlaghai.” Likawa nini? Likawa “mtawala pamoja na Mungu,” *Israeli*. Yeye alishinda.

180 Na Simba huyu wa kabila ya Yuda alishinda. Yeye alisema, “Usilie, Yohana. Kwa maana Simba aliye wa kabila ya Yuda, Shina la Daudi, ameshinda. Yeye ametiisha tayari. Amefanya hivyo. Imekwisha, Yohana.” Whiu! Loo, loo, jamani! Yeye alitoa kitakasaji ambacho kinarudisha dhambi kwenye mikono michafu ambayo ninii. . . kwa hekima yake, iliyomtia unajisi, mwanadamu. Naam.

181 Lakini wakati Yohana alipogeuka kuangalia, alimwona Mwana-Kondoo. Ni tofauti jinsi gani na Simba! Yeye alisema, “Simba ameshinda.” Unaona, tena, ninaweza kutumia hilo hapo, Mungu akijificha katika urahisi. Yeye alisema, “Kuna Simba.” Huyu ndiye yule mfalme wa wanyama. “Simba ameshinda.” Kitu chenye nguvu sana kuliko vyote vilivyoko ni simba.

182 Nimelala huko katika misitu ya Afrika, na kusikia twi—twiga wakilia. Na—na ndovu mkubwa, mwenye nguvu nyingi, huku ameinua mkonga wake hewani, “Whii, whii, whii.” Na kuwasikia watu wa—wa—wakatili waishio jangwani wakipiga kelele zao za kutisha na za kumwaga damu. Na me—mende, mpaka. . . Na mimi na Billy Paul tumelala katika kijibanda kichakavu kilichofunikwa kwa miti yenye miiba. Na kusikia, huko mbali kabisa, simba akinguruma, na kila kitu humo nyikani kinanyamaza. Hata mende wanaacha kupiga makelele. Mfalme anazungumza. Loo, loo, loo, loo, jamani!

183 Ninawaambia, huo ndio wakati madhehebu na mashaka yanapoanguka chini. Kila kitu hunyamaza wakati Mfalme anapozungumza. Na *Huyu* ndiye huyo Mfalme, yaani Neno Lake. Loo!

184 Akasema, “Yohana, usione wasiwasi. Usilie. Usivunjike moyo, Yohana. Niko pamoja na wewe hapa katika ono; ninakuonyesha jambo fulani. Nami najua umehuzunika sana, kwa sababu, unajua, hakuna kitu kitakachokombolewa, kila kitu kimepotea; hakuna mtu angaliweza kutimiza sharti hilo. Lakini Simba aliye wa Kabila ya Yuda. . .”

185 Unajua, Yuda. . . Tulikuwa na jambo hilo, na kwenye ubao hapa, unajua. Kabila ya Yuda, bendera yake, ilikuwa ni simba.

186 Kumbukeni, simba, na—na ndama, na ninii. . . na kadhalika, kichwa cha mwanadamu, na kadhalika. Nao wakiangalia, hao Maserafi, hilo Neno; wakati hao wote, Marko, Mathayo, Luka, na Yohana, wote walikiunga Kitabu cha Matendo.

187 Basi nilimsikia mtu fulani akisema, mhudumu maarufu, akisema, “Kitabu cha Matendo ni fremu tu.”

188 Kilikuwa ndio Mzabibu wa kwanza ambao Kanisa takatifu lilipata kuzaa. A-ha! Naam, bwana. Na kama likipata kuzaa mwingine, utakuwa wa aina hiyo, pia. Naam, bwana! Mna mizabibu iliyopandikizwa, nayo inazaa malimau. Yanapaswa kuwa ni machungwa. Lakini . . . Unaona? Wakati Mzabibu huo—Mzabibu huo ukipata kuzaa tawi Lake tena, utakuwa tu kama lile la asili kabisa.

189 Na Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, Injili hizo zinasimama pale zikilinda Hicho. Hekima ya mwanadamu; nguvu za simba; kazi ya ndama; na wepesi wa chui . . . ama wa tai, hasa. Naam, zile Injili zikisimama pale! Ni nini? Mnakumbuka wakati tulipokuwa nalo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Liko katika *Nyakati Saba za Kanisa*.

Sasa yeye alisema, “Simba aliye wa kabila ya Yuda.”

190 Kwa nini atoke Yuda? “Ee Yuda, mfanya sheria hataitangulia, kati ya magoti yake, hata atakapokuja, Yeye Mwenye Milki. Lakini atakuja kupitia kwa Yuda.”

191 “Na yule Simba, alama ya kabila ya Yuda, ameshinda. Yeye ametiisha.”

192 Na wakati alipoangalia pande zote kuona huyo Simba alipo, alimwona Mwana-Kondoo. Ajabu hiyo, anaangalia aone Simba na anamwona Mwana-Kondoo. Yule mzee alimtaja Yeye kama Simba. Lakini wakati Yohana alipotazama, aliona Mwana-Kondoo, “Mwana-Kondoo kama aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Mwana-Kondoo aliyechinjwa. Ilikuwa ni nini? Huyo Mwana-Kondoo alikuwa ni nini? Alikuwa amelowa damu, amejeruhiwa. “Mwana-Kondoo aliyekuwa amechinjwa, bali alikuwa hai tena.” Naye alikuwa amelowa damu. Loo, jamani!

Mnawezaje kumwangalia Huyo, jamani, na mbaki wenye dhambi?

193 Mwana-Kondoo akatokea. Yule mzee akasema, “Simba ameshinda, Simba wa kabila ya Yuda.” Ndipo Yohana akaangalia amwone huyo Simba, na akaja Mwana-Kondoo, akitetemeka, amelowa Damu, majeraha. Ameshinda tayari. Ungeweza kujua alikuwa vitani. Alikuwa amechinjwa, lakini alikuwa hai tena.

194 Yohana hakuwa amemwona Mwana-Kondoo huyu hapo awali, unajua, hapa. Hakuwa ametajwa kabla. Hakuwa ametajwa mahali popote. Yohana hakumwona, kote Mbinguni, alipokuwa akiangalia. Lakini huyu hapa anajitokeza.

195 Angalia mahali Yeye alipotokea. Alitoka wapi? Alitoka kwenye Kiti cha Enzi cha Baba, ambapo alikuwa ameketi tangu alipochinjwa na kufufuka tena. “Alifufuka na kuketi katika

mkono wa kuume wa Mungu, akiwa hai sikuzote ili atuongee.” Amina. Amesimama pale, leo, kama Mpatanishi, akiwa na damu Yake Mwenyewe, kupatanisha juu ya ujinga wa watu. Sasa, huyo Ndiye ninayemtegemea. Angalia, alikuwa angali amefunikwa na kile kitakasaji, kile kitakasaji cha msamaha wa dhambi.

¹⁹⁶ Yohana akamwanguka huyo Mwana-Kondoo, na huyo Mwana-Kondoo alionekana kana kwamba alikuwa amechinjwa. Kisha akaona ya kwamba alikuwa amejeruhiwa, na kukatwa, na kuchubuliwa, na kutoka damu. Mwana-Kondoo aliyelowa damu, huyo ndiye aliyepachukua mahali petu. Si ni ajabu, ilimbidi Mwana-Kondoo mnyenyekevu kupachukua mahali petu? Naye alimwona huyo Mwana-Kondoo. Alitoka nje.

¹⁹⁷ Yohana hakuwa amemwona, kwa sababu alikuwa huko mbali sana katika Umilele, hata kufanya upatanisho; na kuonyesha ya kwamba hao waliokuwa wamemjia Mungu, chini ya matoleo ya damu ya mafahali, ya mbuzi, dhabihu ya kbadala, Yeye pia. . .Maana, hao walioamini jambo hilo, walielekeza Kwake. Nayo ile Damu haikuwa imemwagwa bado, kwa hiyo Yeye alikuwa pale kuwasafisha. Alikuwa pale kunitakasa mimi na wewe.

¹⁹⁸ Na, Ee Mungu, ninatumaini yuko hapa usiku wa leo. Kwa ajili ya kila mwenye dhambi, Mwana-Kondoo amekwisha chinjwa. Yehova anawezaje kuona jambo lo lote ila huyo Mwana-Kondoo aliyelowa damu aliyesimama pale!

¹⁹⁹ Naye yule Mwana-Kondoo akatoka akaingia kwenye lile ono sasa, kama aliyechinjwa. Angalia, anatoka kwenye Kiti cha Enzi cha Baba. Loo, wazia! Yeye, Yeye alitoka wapi, alipoingia kwenye ono hili? Alitoka Utukufuni, ambako ameketi katika mkono wa kuume wa Mungu. Alitokea mbele, akaenda kwa Yohana, kutoka Utukufuni.

²⁰⁰ Loo, si lingekuwa ni jambo la utukufu kama mawazo yetu machafu, usiku wa leo, yangewekwa kando kirefu vya kutosha kumkubali Yeye, Naye angekuja kutoka huko kote Utukufuni, usiku wa leo, kujijulisha Mwenyewe kwa ye yote wenu!

²⁰¹ Mwana-Kondoo akija kutoka Utukufuni, kwa ajili ya upatanisho, vema, kufanya madai sasa kwa ajili ya ukombozi Wake! Kumbukeni, Yeye alikuwa katika kazi Yake ya upatanisho *huku* nyuma. Lakini, kumbukeni, Mihuri hii iko karibu na kufunguliwa, Na Mwana-Kondoo anatoka kwenye madhabahu ya Mungu, anasogea mbele.

²⁰² Ngojeni mpaka tutakapofika kule, ile saa moja, tuchukue hiyo “nusu saa” ambayo ni kimya. Madhabahu inafuka moshi. Hakuna upatanisho tena. Dhabihu imeondoka. Ni Kiti cha Hukumu. Hakuna Damu juu yake tena, kwa maana Mwana-Kondoo aliyefunikwa na Damu ameondoka. Usingojee mpaka wakati huo. Mnakumbuka katika Agano la Kale? Mradi tu ile damu haikuwa katika kiti cha rehema, ilikuwa ni hukumu; lakini

maradi tu damu ilikuwa pale, kulikuwako na rehema. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tano—Mh.] Lakini wakati Mwana-Kondoo alipoondoka, ilikwisha!

²⁰³ Yeye amekuwa kitu gani? Amekuwa Mpatanishi. Hakuna mtu mwingine! Niambie ambapo Mariamu angefanya upatanisho basi. Mariamu angeweza kutoa nini? Mtakatifu Francis angeweza kutoa nini, Mtakatifu Assisi, ama ye yote yule, na Mtakatifu Cecilia, hasa, ama mwanadamu mwingine ye yote angetoa nini? Yohana hakuona kamwe watakatifu elfu moja wakitoka katika upatanisho. “Yeye aliona Mwana-Kondoo, Mwana-Kondoo aliyechinjwa, amelowa damu.” Sijali ni watakatifu wangapi wamechinjwa; wote walistahili jambo hilo, kila mmoja wao. Kama vile yule mwizi alivyosema pale msalabani, “Tumefanya dhambi, nasi tunastahili jambo hili. Lakini Mtu huyu hajafanya kitu.” Yeye alikuwa ndiye Mtu pekee aliyestahili.

²⁰⁴ Huyu hapa anakuja, kutoka kwenye jukwaa la upatanisho. Anakuja kufanya nini sasa? Mwangalie! Loo! loo! loo! jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu—Mh.]

²⁰⁵ Yohana alikuwa analia. Yote yako wapi yote? Itakuwaje?

²⁰⁶ Kasema, “Usilie, Yohana,” kasema yule mzee. “Huyu hapa Simba anakuja. Ndiye aliyeshinda.” Alipoangalia, huyu hapa Mwana-Kondoo anakuja, amelowa damu, aliyekuwa amechinjwa.

²⁰⁷ Kitu cho chote kinachouawa hulowa damu. Mwajua, kimeuawa. Shingo yake imekatwa, ama cho chote kile. Amejaa damu kila mahali.

²⁰⁸ Huyu hapa Mwana-Kondoo anakuja, aliyekuwa amechinjwa. Naye alikuja kutoka, loo, jamani, (ati nini?) kufanya madai yake juu ya ukombozi Wake. Amina. Loo! Loo! Mimi . . . Wewe hujisikii kama tu kwenda kwenye kona moja, uketi chini na kulia kidogo? Huyu hapa Mwana-Kondoo anakuja, akiwa angali amelowa damu. Yohana . . . Hapakuwapo na kitu pale; watu wote mashuhuri walikuwa wamezunguka mahali pale, bali hapakuwepo na mmoja wao angaliweza kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, huyu hapa Mwana-Kondoo anakuja, sasa. Siku Zake za upatanisho zimekwisha, zile siku za upatanisho.

²⁰⁹ Huo ndio wakati Malaika huyu atakaposimama pale. Wewe ngoja mpaka tutakapofikia kwenye ile Mihuri. “Na hapatakuwa na wakati baada ya haya.” Hiyo ni kweli. Hicho “kimya cha nusu saa.” Angalia jambo linalotukia katika kimya hicho cha nusu saa, wakati huo Muhuri wa Saba, Jumapili ijayo usiku, Bwana akipenda.

²¹⁰ Yeye anakuja (kwani?) kuchukua madai Yake sasa. Loo, jamani! Anakuja kutoa madai Yake! Sasa, Yeye alikuwa amefanya kazi ya Jamaa wa Karibu. Alikuwa ameshuka,

akawa Mtu, akafa. Alifanya kazi ya ukombozi ya Jamaa wa Karibu, lakini alikuwa bado hajatoa madai yake. Sasa anatokea jukwaani kudai haki zake, (angalia kinachotukia) loo! jamani, ambayo yalimfanya auawe, kwa kufanyika Jamaa wa Karibu wa mwanadamu, apate kufa mahali pake, kumkomboa. Lakini, yule mzee alisema kweli aliposema Yeye alikuwa ni “Simba,” mnaona. Yule mzee alimwita Yeye, kasema, “Simba.” Kwa sababu, Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo, Mpatanishi, Mwana-Kondoo aliyelowa damu, lakini sasa Yeye anakuja kama Simba. Siku Zake za upatanisho zimekwisha.

²¹¹ “Mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu. Mwenye haki na azidi kufanya haki. Mtakatifu na azidi kutakaswa.” Jambo hilo limefungwa. Loo, ndugu! Halafu? Halafu nini?

²¹² Na, kumbukeni, jambo hilo linakuja kwenye wakati wa saba wa kanisa, wakati siri za Mungu zitakapofunguliwa. Sasa angalia kwa makini sana. Hili ni jambo unalopaswa kulipata. Sasa, Yeye alikuwa akifanya kazi Yake ya upatanisho, akimwombea mwamini. Kwa miaka elfu mbili aliyokuwa Mwana-Kondoo, huko nyuma. Sasa Yeye anatoka kuja kutoka katika Umilele, kukitwaa kile Kitabu cha hati-miliki, na hati ya kumiliki, na kuivunja ile Mihuri, na kuzifunua zile siri. Wakati gani? Kwenye wakati wa mwisho.

²¹³ Mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, tutaendelea mbele basi.

²¹⁴ Sasa, kuvunja ile Mihuri na kuwafunulia siri zote, kumfunulia malaika wa saba, ambaye Ujumbe wake ni kufunua siri zote za Mungu. Siri za Mungu ziko kwenye hii Mihuri Saba. Unaona? Hivyo ndivyo alivyosema hapa. Siri zote ziko katika hii Mihuri Saba.

²¹⁵ Naye Mwana-Kondoo anatokea sasa, anaacha kuwa Mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu. Anakuwa Simba. Na wakati anapokuwa Simba, anakitwaa kile Kitabu. Hizo ni haki Zake. Mungu alikishikilia, ile siri, lakini sasa yule Mwana-Kondoo anakuja.

²¹⁶ Hakuna mtu angeweza kukitwaa kile Kitabu. Kingali kiko katika mikono ya Mungu. Hakuna papa, kasisi, cho chote kile, hawawezi kukitwaa (la) kile Kitabu. Ile Mihuri Saba haijafunuliwa. Unaona?

²¹⁷ Lakini wakati, yule Mpatanishi, wakati kazi Yake imekwishafanywa kama Mwombezi, anatokea. Na Yohana... Yule mzee alisema, “Yeye ni Simba.” Naye anajitokeza. Mwangalie. Loo, jamani! Unaona? Yeye anajitokeza kukitwaa kile Kitabu, sasa angalia, kuzifunua siri za Mungu, ambazo wengine wamezibuniabunia, katika nyakati hizi zote za kimadhehebu.

²¹⁸ Unaona, basi, yule malaika wa saba. Kama kitabu hiki, siri, ni Neno la Mungu, yule malaika wa saba hana budi kuwa ni

nabii, kujiwa na Neno la Mungu. Hakuna cha makasisi, mapapa, au cho chote kile, kiwezacho kulipata; Neno haliwajilii watu kama hao. Neno la Mungu humjia nabii tu, daima. Malaki 4 iliahidi jambo hilo. Na wakati atakapotokea, atazichukua siri za Mungu, ambapo kanisa lilikuwa limetatanikiwa kabisa katika madhehebu haya yote, “Na kuirudisha Imani ya watoto iwaelekee baba zao.” Na ndipo hukumu ya ulimwengu itashuka, na ulimwengu utachomwa moto. Halafu wenye haki watatembea juu ya majivu ya walio waovu, katika ule Utawala wa Miaka Elfu.

219 Mnalipata jambo hilo sasa? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Vema.

220 Wengine walikuwa wamelibunia jambo hilo, katika wakati wa kimadhehebu. Lakini, unaona, hana budi kuwa ni mtu huyu, yule malaika wa saba wa . . . Ufunuo 10:1-4 ni nanii. . . Yule malaika wa saba amepewa siri za Mungu, na anamaliza siri zote ambazo ziliachwa, kote katika nyakati za kimadhehebu.

221 Sasa unaweza kuona ni kwa nini siwashambulii ndugu zangu walio katika madhehebu. Ni ule utaratibu wa kimadhehebu! Hawaninii, hawana haja ya kujitahidi kujua Hilo, kwa sababu halingeweza kufunuliwa. Hiyo ni kulingana na Neno. Walilidhania, na kuamini lilikuwapo, na kwa imani wakatembea Kwalo, lakini sasa limethibitishwa dhahiri. Amina. Loo, jamani, ni—ni Andiko la namna gani!

222 Sasa angalia. Basi ni Yeye, yule Mwana-Kondoo, anayechukua mahali pake pa Kifalme, wakati watakatifu Wake watakapokuja kumvika Yeye taji, “Bwana wa bwana, Mfalme wa wafalme.” Unaona?

223 Unaona, “Wakati umekwisha.” Ufunuo 10:6, “Hapana wakati tena.”

224 Angalia, kuna “pembe saba” juu ya Mwana-Kondoo huyu. Mliona jambo hilo? “Mwenye pembe saba.” Ndiyo kwanza tupitie jambo hilo. *Pembe* zinamaanisha “nguvu,” kwa mnyama. Pia, angalia, Yeye hakuwa mnyama, kwa sababu alikitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi. Unaona? Angalia. Loo, jamani!

225 Ninaamini niliandika jambo hilo mahali fulani; loo, kuvunja ile Mihuri, na kufungua ile hati, ile hati-miliki, na ule—ule Ujumbe kwa malaika wa mwisho. Naye anaketi katika mahali Pake pa Kifalme. Hicho ndicho anachokuja sasa kufanya.

Sasa angalia, wakati Yeye anapotoka, “Zile pembe saba.”

226 Sasa, wakati alipomwona Mwana-Kondoo huyu, Yohana akimwangalia, ali—alionekana kana kwamba amechinjwa, ametapakaa damu. Naye ametokea Umilele, Naye akaacha kuwa Mpatanishi.

227 Basi wewe omba kwa Mariamu kadiri utakavyo! “Hakukuwako na mtu Mbinguni, na duniani, ama hapana mtu, hakuna mwenye uhai mahali po pote, angeweza kukitwaa.” Yohana hata alilia kwa ajili ya jambo hilo. Loo! rafiki Mkatoliki, je! huwezi kuona jambo hilo? Usimwombe mtu fulani aliyekufa.

228 Mwana-Kondoo ndiye Mpatanishi pekee. Unaona? Yeye ndiye aliyejitokeza. Basi alifanya nini sasa? Alikuwa nyuma huku akifanya upatanisho, mpaka Damu Yake imepatanisha kwa kila mtu. Naye Mwana-Kondoo, sasa, anajua yale yaliyoandikwa katika kile Kitabu. Kwa hiyo, Yeye alijua tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu majina yao yalikuwa Mle ndani, kwa hiyo Yeye amesimama hapa nyuma na kuninii. . . na—na, lakini, akafanya kazi ya Mpatanishi namna hii mpaka. . . kazi ya upatanisho, mpaka kila mtu aliyewekwa kwenye kile Kitabu amekombolewa, na imekwisha. Na sasa Yeye anatoka. Unaona? Amekwishafanya kazi yake ya Jamaa wa Karibu. Yeye ameninii kabisa. . . Unajua kazi ya Jamaa wa Karibu ilikuwa ni nini? Kushuhudia mbele ya wazee. Mnakumbuka Boazi akitoa kiatu chake, na kadhalika? Yeye amefanya haya yote sasa.

229 Sasa Yeye anakuja kumchukua Bibi-arusi Wake. Amina. Anakuja sasa kama mfalme. Anamtafuta Malkia Wake. Amina. Amina. Katika Kitabu hiki ndimo mlimo na siri yote ya Hilo, imeviringishwa katika ninii, katika Mihuri Saba. Loo, ndugu! Mihuri Saba, ikimngojea Yeye aje. Angalia.

230 Hebu na tupate mifano hii. Vema, ni saa tatu tu. Tumebakiza masaa matatu ama zaidi, yaliyotusalia. Tuna. . . hebu ninii tu. . . Shetani anakaza kuniambia watu hao wanachoka, kwa hiyo nafikiri wanachoka. Lakini hebu—hebu na tuchukue jambo hili, hata hivyo.

231 “Pembe Saba” zilikuwa ni yale makanisa saba, unaona, zile nyakati saba za kanisa, kwa sababu hizo zilikuwa ndizo ulinzi wa Mwana-Kondoo. Alizolinda kwazo haki zake, duniani, ilikuwa ni Kundi la watu waliotumwa na Mungu ambao walilinda; unaona, ile pembe juu ya Mwana-Kondoo.

232 “Macho saba” ni wale wajumbe saba wa zile nyakati saba za kanisa. “Macho saba,” waangalizi saba.

233 Je! mngependa kuandika Maandiko machache? Hebu na tuyafungue tu hayo. Mnasemaje, mna wakati kama huo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Vema. Hebu na twende katika Zekaria, Kitabu cha—cha Zekaria, kidogo tu, nasi tuta—tutasoma sehemu ya haya.

234 Si—sitaki kuwachelewesheni sana katika mambo haya. Na—nami. . . Lakini, hata hivyo, sitaki mlikose. Ni kitu gani kilicho muhimu zaidi kuliko jambo hili? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Naam. Ni kitu gani. . . [Mtu fulani katika kusanyiko anasema, “Ndugu Branham?”] Naam? [“Usiupime huo.”] Hakuna kitu kilicho muhimu kuliko Uzima wa Milele kwa

mtu. Nasi hatuna—hatuna budi kupata jambo hili sasa, na—na tuwe na hakika ya kwamba tunalipata. Vema. Vema, bwana.

235 Na sasa tunataka kusoma Zekaria sura ya 3. Nadhani hiyo ndiyo, sasa, Zekaria 3. Tutaenda tu kuchukua mifano hii hapa, kama nimeandika Maandiko yangu. Nilikuwa nikipiga viyowe vya furaha kila mahali, adhuhuri ya leo, nilipopata jambo hili. Kwa hiyo si—sijui tu kama nimeyaandika sawasawa, ama la. Ninatumaini nimefanya hivyo. Zekaria 3, hebu na tuone kama ni . . . Nina 89 hapa, lakini haina budi kuwa ni 8 hadi 9. Sawa. Sawa. Ninajua haiwezi kuwa 89. Zekaria 3:8 na 9.

Sikiliza sasa, Ee Yoshua, kuhani mkuu, wewe na wenzako waketio mbele yako; maana hao ni watu walio ishara; kwa maana, tazama, ninamleta mtumishi wangu, aitwaye CHIPUKIZI (Kristo).

Maana, litazame jiwe hili nitakaloliweka mbele ya Yoshua; katika (jiwe) jiwe moja yako macho saba, (macho saba), tazama, nitachora machoro yake, asema BWANA wa majeshi, . . . nitauondoa uovu wa nchi ile katika siku moja.

236 Sasa hebu na tufungue Zekaria 4:10, 4:10. Sikilizeni.

. . . ni nani aliyeidharau siku ya mambo madogo (Mungu katika urahisi, unaona)? kwa kuwa watafurahi, nao wataiona timazi katika mikono ya Zerubabeli; ambaye ninii yake . . . naam, hizi saba, hizi ndizo macho ya Bwana; yapiga mbio huko na huko duniani mwote.

237 “Yale macho saba.” Macho maana yake ni “kuona.” Kuona maana yake ni “manabii, waonaji.” Mwana-Kondoo huyu alikuwa na pembe saba, na kila pembe ilikuwa na jicho, “macho saba.” Ni kitu gani? Kristo na Bibi-arusi Wake; nyakati saba za kanisa. Kutoka katika hizo kulitokea manabii saba, waonaji saba, macho. Kwa hiyo, yule wa mwisho hana budi kuwa ni nabii. Ndugu Branham aligonga kwenye mimbara mara mbili aliposema, “mwonaji.”—Mh.] Vema.

238 Angalia, Yeye si mnyama. “Alikitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa kuume Wake Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi.” Alikuwa ni nani? Yule—yule Mwenyewe, yule Mwenyewe wa asili, aliyekuwa na kile Kitabu cha Ukombozi katika mkono Wake wa kuume. Wala hakuna Malaika, hakuna Kiumbe cha Malaika, hakuna cho chote kingine, kingeweza kupachukua mahali hapo. “Naye Mwana-Kondoo huyu aliyelowa damu akatoka na kukitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono Wake.” Whiu! Ilikuwa ni nini? Ndugu, hili ndilo jambo lililo tukufu kuliko yote katika Maandiko. Amina. Tendo ambalo hakuna Malaika, hakuna kitu cho chote, kingeweza kulifanya. “Naye Mwana-Kondoo akaja na kukitwaa kutoka katika mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi.”

²³⁹ Ni kitu gani? Sasa ni mali ya Mwana-Kondoo. Amina. Sheria za Mungu zilihitaaji. Yeye Ndiye anayekishikilia. Sheria ya Mungu ilihitaaji Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu. Ndipo Mwana-Kondoo akatokea, amekishika, “Mimi ni Jamaa yao wa Karibu. Mimi ni Mkombozi wao. Sasa mimi. . . Nimewafanyia upatanisho, na sasa nimekuja kudai haki zao kwa ajili yao.” Amina. Huyu ndiye peke Yake. “Nimekuja kudai haki zao. Kwamba, wao wana haki ya kila kitu kilichopotea katika lile anguko, nami nimelipa ile gharama.”

²⁴⁰ Loo, ndugu! Whiu! Hilo haliwafanyi kujisikia wa kiroho ndani? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Si kwa kazi njema ambazo tumefanya, bali kwa neema Yake.”

²⁴¹ Loo, ngoja kidogo! Na hao wazee na kila kitu kinginecho wakaanza kutupa taji zao, na watu mashuhuri wakaanza kupomoka chini, unaona.

Hakuna, hakuna mtu angaliweza kufanya jambo hilo.

²⁴² Naye anaenda moja kwa moja hadi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, na kukitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono Wake, na kudai haki Zake. “Nimewafia. Mimi ndiye Mkombozi aliye Jamaa yao wa Karibu. Ni Mimi. Mimi ndimi Mpatanishi. Damu Yangu ilimwagwa. Nimefanyika Mtu. Nami nilifanya jambo hilo kusudi nilirudishe Kanisa hilo tena, lile nililoona kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Nimelikusudia. Nililina, lingekuwako. Na hakuna mtu aliyeweza kukitwaa, bali nilishuka nikaenda nikafanya jambo hilo, Mimi Mwenyewe. Mimi ndiye Jamaa yao wa Karibu. Nilifanyika wa ndugu yao.” Ndipo anakitwa kile Kitabu. Amina!

²⁴³ Loo, Ni nani anayeningojea Kule usiku wa leo? Ni nani Huyu, enyi kanisa, anayeningojea Kule? Ni kitu gani kingine kingeweza kukungojea Kule? Yule Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu! Loo, jamani! Ni tamshi la fahari jinsi gani, ama tendo!

²⁴⁴ Sasa Yeye ana hati-miliki ya ukombozi. Anayo katika mkono Wake. Upatanisho umekwisha sasa. Anayo mkononi Mwake. Kumbukeni, ilikuwa katika mkono wa Mungu, wakati wote, lakini sasa iko mkononi mwa Mwana-Kondoo. Sasa angalia. Hati-miliki ya ukombozi, wa viumbe vyote, iko katika mkono Wake. Naye amekuja kuidai airudishe, pia, kwa ajili ya jamii ya binadamu. Si kuidai irudi kwa Malaika. Aliidai iwarudie wanadamu, ambao walipewa hiyo, kuwafanya wana na binti za Mungu tena; kuwarudisha tena katika bustani ya Edeni, kila kitu walichopoteza; viumbe vyote, miti, uhai wa wanyama, kila kingine kile. Loo, jamani!

²⁴⁵ Hilo haliwafanyi kujisikia wenye furaha? Whiu! [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nilidhani nilikuwa nimechoka, lakini sasa sijachoka. Unaona? Wakati mwingine ninafikiri nina—ninakuwa mzee mno kuweza kuhubiri, halafu ninaenda kuona

kitu kama hicho, nami ninafikiri mimi ni kijana tena. Naam. Aha. Aha! Linafanya jambo fulani kwako. Unaona?

²⁴⁶ Kwa kuwa ninajua jambo hili, ya kwamba kuna Mtu Fulani Kule anayeningojea. Kuna Mtu aliyelipa deni ambayo nisingeweza kulipa. Hiyo ni kweli. Yeye alinilipia, Charlie. Alikulipia. Aliilipia jamii yote ya binadamu. Na sasa anakuja kudai haki Zake za ukombozi. Kuzidai kwa ajili ya nani? Si kwa ajili Yake; kwa ajili yetu. Yeye ni mmoja wetu. Yeye ni jamaa yetu. Loo, jamani! Yeye ni Ndugu yangu. Yeye ni Mwokozi wangu. Yeye ni Mungu wangu. Yeye ni Mkombozi wangu aliye Jamaa wa Karibu. Yeye ni yote. Kwa kuwa Mimi nilikuwa ni kitu gani bila ya Yeye, ama ningekuwa kitu gani bila ya Yeye? Kwa hiyo, unaona, Yeye ni Yote kwangu. Naye anasimama Pale kama jamaa zetu. Na sasa amekuwa akituombea, hadi kufikia wakati huu. Na sasa Yeye anatokea na kukichukua Kitabu cha Ukombozi, kudai haki Zake, za ya yale aliyotufanyia.

²⁴⁷ Wao wanakufa. Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, ingawa alikuwa amekufa, hata hivyo ataishi. Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Yeye aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa milele, Nami nitamfufua katika siku ya mwisho.”

²⁴⁸ Haidhuru, akilala mauti katika zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, ama ya saba, po pote atakapolala mauti. Itakuwaje? Parapanda ya Mungu italia. Ile parapanda ya mwisho italia, wakati ule ule yule malaika wa mwisho anapotoa Ujumbe wake na Muhuri wa mwisho unafunguliwa. Ile parapanda ya mwisho italia, ndipo Mkombozi anakuja kuchukua mali yake iliyokombolewa, Kanisa Lake, lililosafishwa kwa Damu.

²⁴⁹ Sasa, loo, viumbe vyote vimo katika mkono Wake sasa, ambamo mpango wote wa ukombozi umetiwa muhuri kwa Mihuri saba ya siri, katika Kitabu hiki alichokitwaa. Sasa angalia. “Na Yeye Pekee ndiye tu anayeweza kumfunulia ye yote atakaye.” Amekishika katika mkono Wake, unaona. Sasa, Yeye aliahidi kitafunuliwa wakati huo, sasa, kwa kuwa kimetiwa muhuri kwa Mihuri Saba ya siri, kile Kitabu cha Ukombozi. Sasa angalia. Kama vile sasa . . .

²⁵⁰ Enyi marafiki, niliwaambia, nitawaachilia mtoke kwenye saa mbili na nusu, lakini nimerusha kurasa tatu ama nne hapa, nipate kufikia jambo hili. Kwa hiyo ninataka . . . Nimeshavuka saa tatu. Ili kwamba mpate kurudi kesho.

²⁵¹ Lakini sasa katika Kitabu hiki cha Mihuri saba, cha ukombozi, ambacho Mwana-Kondoo alikitwaa, ndani Yake Mwenyewe, alikuwa Ndiye pekee Ambaye angaliweza kufanya jambo hilo. Naye alikitwaa kutoka katika mkono wa kuume Wake Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi, sasa, kudai ninii Zake za ukombozi, kudai haki Zake. Kudai, kwa ajili

yangu na kwa ajili yako, kile alichotukombolea, kuninii, unaona, kuturudisha kwenye kila kitu ambacho Adamu alipoteza katika bustani ya Edeni. Yeye ametukomboa kuturudisha katika hayo.

²⁵² Sasa pamoja na Mwana-Kondoo, akiwa na kile Kitabu mikononi Mwake, tuko tayari kuomba neema na rehema Zake juu yetu, kutufungulia hiki Kitabu cha Mihuri Saba, na aturuhusu tuangalie ng'ambo ya pazia la wakati, kidogo tu. Loo, jamani! Angalia wakati alipokitwaa kile Kitabu, ile hati-miliki, iliyotiwa muhuri, (shika hilo tu niani mwako sasa), na kuivunja ile Mihuri ya ile siri, kuifunua, kuileta kwa nanii Wake, unaona, raia Wake wote waliokombolewa.

²⁵³ Sasa, tutakapofikia jambo hili katika ile Mihuri, tutarudi kule nyuma na kuona hizo nafsi zilizo chini ya madhabahu, zikilia, “Bwana, hata lini, hata lini?”

²⁵⁴ Na hapa Yeye ni kama Mpatanishi, kwenye madhabahu, “Muda kidogo tu, mpaka kutakapokuwa na wengine itakaowabidi kuteseka kama ninyi.”

²⁵⁵ Lakini sasa anatoka hapa, kwenye Muhuri huu wa mwisho. Yeye si Mpatanishi tena. Yeye ni Mfalme sasa. Naye anafanya nini? Kama Yeye ni Mfalme, hana budi kuwa na raia. Na raia Wake ni wale ambao amewakomboa, nao hawawezi kumkaribia mpaka atakapochukua zile haki za ukombozi. Na sasa Yeye anakwenda, kutoka kuwa Mpatanishi; ambapo mauti ilituweka katika kaburi, Yeye anatoka akiwa na haki Zake. Amina.

²⁵⁶ “Na hata wale walio hai na kusalia mpaka Kuja Kwake, hawatawazuia wale waliolala mauti. Kwa kuwa parapanda ya Mungu italia, kwenye ile parapanda ya mwisho.” Wakati Muhuri wa mwisho utakapovunjwa, na wakati yule Malaika wa saba anapotangaza Ujumbe wake, “Parapanda ya mwisho italia, na waliokufa katika Kristo watafufuka. Na sisi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, kumlaki Yeye hewani.” Yeye anadai! Yeye amekuja sasa kudai mali Ya—Yake.

²⁵⁷ Angalia! Angalia jambo hili! Jamani! Akavunja ile Mihuri, akafunua zile siri. Akazifunua (wapi?) kwa wakati wa mwisho wa kanisa, ambao ndio pekee wanaoishi. Wengine wao wamelala.

²⁵⁸ Yeye alisema, “Kama akija katika zamu ya kwanza, zamu ya pili, zamu ya tatu, na kuendelea mpaka zamu ya saba.” Katika zamu ya saba, a—amri ilitolewa, ama wito, “Tazama, Bwana arusi yuaja!”

²⁵⁹ Na wakati walipoambiwa jambo hilo, yule bikira aliyelala, yale makanisa baridi, yalisema, “Loo, unajua, ni—naona ningetaka kumpokea huyo Roho Mtakatifu.” Mmewaona Wapresbiteri na Waepiskopalia? Mlisikia Ujumbe wangu huko Phoenix, kwa hao watu wanaosimama kule, katika lile gazeti la *Voice* na pale ninii, nikisema...Vema, nini kimempata mwandishi huyu, anayesema, “Baba Mtakatifu *Fulani*”? Wakati,

Biblia ilisema, “Msimwite mtu ye yote, ‘Baba,’ namna hiyo.” Unaona, wao wanalala pamoja nao, hiyo ndiyo sababu, lakini wakati walipokuja na kusema, “Naam, tunaamini.”

260 Mwanamke mmoja alimpigia simu mwanamke mwingine sasa hivi, kasema, “Unajua, mimi ni Muepiskopalia.” Kasema, “Ni—ni—nilinena kwa lugha, hivi majuzi. Ninaamini nilimpokea Roho Mtakatifu, lakini, sh, usimwambie mtu.” Ninashuku jambo hilo sana. Huenda ulinena kwa lugha. Lakini, kama umeuwasha moto moyo wa mtu, mtu huyo atatuliaje? Hiyo ni kweli. Unaona? Unaona? Hawezi kutulia.

261 Ungeweza kuwawazia akina Petro, na Yakobo, na Yohana, na hao wengine kule juu kwenye chumba cha juu, wakisema, “Loo, tuna Roho Mtakatifu sasa, lakini labda ni afadhali tutulie tu”? Ndugu, kupitia madirishani, milangoni, na kila kitu, hao wakatoka, wakaingia mitaani, wakiwa kama kundi la walevi. Huyo ndiye Roho Mtakatifu halisi.

262 Lakini, unaona, huyo mwanamwali aliyelala hapati kitu cho chote, hata hivyo. A-ha. Hiyo ni kweli. Pia kumbukeni, wakati walipotoka kwenda kununua Mafuta, kumbukeni, Maandiko hayasemi waliyapata.

263 Lakini wakati walipokuwa wametoka kwenda kujaribu kuyanunua, kulitokea sauti. Ni nini kilichotukia? Wanawali wote wale waliolala, walianka na kusafisha taa zao, “na wakaingia kwenye ile Karamu.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

264 Na hao wengine waliachwa kwa kipindi kile cha Dhiki, kweli, “Wakilia, wakiomboleza, na kusaga meno.” Hilo ni kanisa, si Bibi-arusi; kanisa.

265 Bibi-arusi aliingia. Kuna tofauti kubwa sana kati ya kanisa na Bibi-arusi. Naam, bwana! A-ha. “Wakaingia katika Karamu ya Arusi.” Loo, angalia, jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.]

266 Ile Mihuri ilivunjwa (kwa nini?) katika wakati wa mwisho wa kanisa, kufunua Kweli hizi. Kwa nini? Mwana-Kondoo alivunja hiyo Mihuri na kuifunua kwa Kanisa Lake, kusudi apate kuwakusanya raia Wake kwa ajili ya Ufalme Wake. Bibi-arusi Wake, unaona! Loo, jamani! Yeye anataka kuwaleta raia Wake Kwake sasa.

267 Ni nini? Kutoka katika mavumbi ya dunia, kutoka katika kilindi cha bahari, kutoka katika mashimo, kutoka kila mahali na kila sehemu, kutoka—kutoka katika sehemu zenye giza, kutoka paradiso, po pote wanapoweza kuwa. Yeye ataita, nao watajibu. Amina! Amina! [Kusanyiko, “Amina.”] Yeye ataita, nao watajibu.

268 Yeye alikuja kuwachukua raia Wake. Yeye alizifunua siri Zake, nao wakazona. “Na hapatakuwa na wakati baada ya haya,” wakati huo. “Wakati umekwisha.” Umekwisha. Vema.

269 Yeye anaondoka kwenye kile Kiti cha Enzi, kuwa Mpatanishi, kama Mwana-Kondoo aliyechinjwa; apate kuwa Simba, Mfalme; apate kuuleta ulimwengu Hukumuni, ambao wameukataa Ujumbe Wake. Yeye si Mpatanishi.

270 Kumbukeni mafundisho ya Agano la Kale sasa, tunapoharakisha. Wakati damu ilipoondolewa kwenye kiti cha rehema, kilikuwa ni nini? Kiti cha Hukumu.

271 Na wakati yule Mwana-Kondoo, aliyechinjwa, alipotoka akaja kutoka Umilele, kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Baba, na kuchukua haki Zake, kilikuwa ni Kiti cha Hukumu. Ndipo Yeye akawa, si Mwana-Kondoo, bali Simba, Mfalme, Naye anamwita Malkia Wake aje asimame karibu Naye.

272 “Hamjui ya kwamba watakatifu wataihukumu nchi?” Danieli alisema, “Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa; na elfu kumi mara elfu kumi ya maelfu wakamtumikia,” Mfalme na Malkia. “Kisha Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa ni Kitabu cha Uzima,” hicho ni cha kanisa. Naye Malkia pamoja na Mfalme wakasimama pale.

273 Kama vile shairi la mchungu ng’ombe lilivyosema:

Jana usiku nilipokuwa nimelala malishoni,
Niliangalia nyota mbinguni,
Nami nilishangaa kama mchungu ng’ombe
wakati wo wote
Angeweza baadaye kuingia kwenye ile raha.

Kuna njia ya kuingia katika Nchi ile
inayong’aa, yenye furaha,
Lakini kuna giza kule, mkondo fulani, ndivyo
wanavyosema,
Lakini ile pana inayoelekeza upotevuni
Yote imepambwa na inang’aa kote njiani.

Wananena juu ya Tajiri mwingine mkuu,

274 Yeye ananena katika lugha ya maisha yake ya uchungaji wa ng’ombe. Kama ulipata kuwa katika kukusanya ng’ombe, ungeweza kuliona kwa dhahiri.

Wananena juu ya Tajiri mwingine mkuu,
Naye kamwe ng’ombe kwake hawafuriki,
ndivyo wasemavyo,
Daima atakuwa na nafasi kwa mwenye dhambi
Atakayeenda katika hiyo njia iliyonyoka, iliyo
nyembamba.

Wanasema Yeye hatakuacha kamwe,
 Naye anajua kila tendo na mtazamo;
 Kwa, kwa ajili ya usalama, afadhali tutiwe
 alama,
 Jina letu liandikwe katika Kitabu Chake kikuu
 cha kuorodhesha.

Kwa kuwa wao wanasema kutakuwa na
 kukusanyika kukuu,
 Wakati wachunga ng'ombe kama ndama
 yatima watasimama,
 Wapate kutiwa alama na wapanda farasi wa
 hukumu,
 (hao manabii na waonaji)
 Waliowekwa kazini na wanajua kila aina.

²⁷⁵ Kama ulipata kuwa katika kukusanya ng'ombe, umwone
 bosu amesimama pale nje, na hao wapanda farasi, na
 kuzungushwa-zungushwa kwenye kundi hilo la ng'ombe.
 Yeye ataona chapa yake ikipita, naye atamwita bosu. Naye
 bosu ataona, na kumwashiria. Ng'ombe wake ataingia moja
 kwa moja, atazunguka, na kuzunguka katika mzunguko huu
 wa kundi la ng'ombe waliokatwa pembe namna hiyo, na
 kuwatenganisha ngombe wake. Unaona?

Wanasema kutakuwa na kukusanyika
 kukubwa,
 Nao wachunga ng'ombe kama ndama yatima
 watasimama,
 Watakaotiwa alama na wapanda farasi wa
 hukumu,
 Waliowekwa kazini na wanajua kila aina.
 (Unaona?)

²⁷⁶ Kwa hiyo alisema:

Nadhani nitakuwa ndama mdogo aliyepotea,
 Mtu tu aliyehukumiwa kifo, asiyetiwa alama,
 (huyo, wanamfanya mchuzi, unaona),
 Atakayetenganishwa na kundi hilo pamoja na
 wajeuri wengine,
 Wakati Bosu wa hao wapanda farasi
 atakapokuja.

²⁷⁷ Mnaona ni nani? Yule Bosu wa hao wapanda farasi. Huyu ni
 Mwana-Kondoo, kwa wale wajumbe saba ambao wamewekwa
 kazini na wanajua kila alama. Unaona? A-ha!

²⁷⁸ Angalia, huyu hapa anakuja. Anaondoka kwenye kile Kiti
 cha Enzi, kama Mpatanishi, kama Mwana-Kondoo aliyechinjwa;
 awe Simba, Mfalme, kuuleta ulimwengu wote katika Hukumu,
 ambao umemkataa. Mkombozi wetu aliye Jamaa wa Karibu
 wakati huo ni Mfalme juu ya wote. Kwa nini? Yeye ana hati-

miliki ya ukombozi. Yote yako katika mkono Wake. Ninafurahi kwamba ninamjua. Unaona?

279 Ndipo anadai urithi Wake; hilo ni Kanisa, Bibi-arusi. Yeye anadai Hilo.

280 Yeye anafanya nini basi? Anammaliza mshindani Wake, Shetani. Anamtupa katika Ziwa la Moto, pamoja na wale wote walioongozwa na Shetani, kulikataa Neno Lake la ukombozi.

281 Yeye ni Mfalme sasa. Rehema ingali iko kwenye kile Kiti cha Enzi. Usikatae Neno Lake. Unaona? Wale wapanda farasi wanajua vizuri wewe ni nani.

282 Na, sasa, mshindani Wake, ambaye amemsumbua kwa muda wa miaka elfu mbili, akidai, “Ninaweza kuwafanyia lo lote nitakalo. Bado wako mkononi mwangu. Wao ni wangu. Mimi . . . Waliipoteza ile hati-miliki kule nyuma.”

283 Lakini Yeye ni Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu. Yeye alisema yuko nyuma hapa akiwaombea sasa. Lakini siku moja . . .

Anasema, “Nitawaweka kaburini.”

284 Lakini Yeye aliliambia Kanisa, “Nitawafufua.” Unaona? “Lakini, kwanza, sina budi kuwa Mwombezi.”

285 Sasa Yeye anatokea, anatoka kutoka katika Umilele kule nyuma mbali, anatoka kwenye kile Kiti cha Enzi cha Baba, ambako aliketi kama Mwombezi. Sasa Yeye anakuja kuwa Mfalme, loo, kutawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Hukumu imewekwa. Loo, ndugu, Mkombozi aliye Jamaa yetu wa Karibu anashikilia yote. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

286 Yeye anafanya nini? Anamsai yule mshindani, Shetani. “Wao ni wangu sasa. Nimewafufua kutoka kaburini.” Kisha anawachukua waongo wote, na wenye kulipotosha Neno, na wote wa namna hiyo, pamoja na Shetani, na kuwaangamiza katika lile Ziwa la Moto. Yote yamekwisha, sasa. Anawatupa katika Ziwa la Moto. Loo, jamani!

287 Mnajua nini? Ninataka—ninataka kusema jambo fulani hapa kabla hatujafunga. Na ndipo tuta—tuta—tutaharakisha. Angalia. Sasa tumefikia kifungu cha 7. Lakini kutoka kifungu cha 8, hadi cha 14, ninataka mwone kile kinachotukia.

Wote waliokuwa *mbinguni*, na wote waliokuwa *juu ya nchi* . . .

288 Hebu sikilizeni tu jambo hili. Hebu nilisome tu sasa. Ninaamini lingekuwa ni jambo bora zaidi kama nikilisoma tu kutoka katika Kitabu, pamoja na kifungu cha 7, unaona. Pia angalieni kifungu cha 6.

Nikaona—ninaona, nikaona, na, tazama, katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa

kana kwamba amechinjwa, mwenye vichwa saba . . . ama pembe saba (namaanisha) pembe saba na macho saba, (tumeeleza hilo sasa hivi), ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote.

289 Mnaona, nyakati saba za kanisa, wale wajumbe saba waliodumisha ule Moto kuwaka. Mnaona? Vema.

Naye akaja (yule Mwana-Kondoo), akakitwa kile kitabu katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi-aliyeketi juu ya kiti cha enzi.

290 Sasa angalia. Na wakati alipofanya hivyo, angalia jambo lililotukia. Nena kuhusu yubile! Sasa huku ndiko kule kuvunjwa hasa kwa hiyo Mihuri, kunatukia. Tutafikia kwenye kile “kimya cha nusu saa,” mara baada ya jambo hili. Angalia jambo hili, nasi tutaanza kuliingilia. Tutamalizia jambo hili, Jumapili ijayo usiku, papa hapa. Na sikilizeni kwa makini sasa. Mko tayari? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sikilizeni kwa makini, jambo lililotendeka wakati alipofanya jambo hili.

291 Wakati viumbe vyote vilipokuwa vinaugua; hakuna aliyejua la kufanya, na Yohana alikuwa analia. “Hapa akaja Mwana-Kondoo, akaenda pale!” Na Kitabu hiki kilikuwa katika mikono ya—ya Mwenyewe wa asili, kwa maana mwanadamu alikuwa ameanguka na kukipoteza. Wala hakuna mtu aliyeweza kukitwaa, tena, kuikomboza dunia; hakuna kasisi, papa, hakuna cho chote, kama nilivyosema. “Lakini Mwana-Kondoo akaja!” Hakuna cha Mariamu, hakuna cha mtakatifu *huyu*, ama cha mtakatifu *yule*. “Mwana-Kondoo akaja, amelowa damu, amechinjwa, na akakitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi.” Na wakati walipoona kulikuwako na Mkombozi; na ninii wote—zile nafsi chini ya madhabahu, wakati Malaika, wakati wale wazee, wakati kila kitu kilipoona jambo hilo, wakati jambo hili lilipotendwa. Lingali, bado, liko katika siku zijazo. Usiku wa leo Yeye ni Mpatanishi, lakini Yeye atafikia jambo hili. Angalia.

Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.

292 Hao ni wale walio chini ya madhabahu, ambao wameomba, kwa muda mrefu zamani. Unaona, walikuwa wameomba wapate ukombozi, wakaomba wapate ufufuo. Na hapa hawa— hawa wazee wanamwaga maombi yao mbele ya . . . Maana, sasa tuna Mwakilishi, tuna Jamaa wa Karibu Mbinguni, ambaye amekuja kutoa madai Yake.

Nao waliimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa

kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu wetu (angalia) kwa damu yako watu wa kila kabila . . . lugha na jamaa na taifa,

Nawe umetufanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nasi tutamiliki juu ya nchi.

293 Walitaka kurudi. Na hawa hapa wanarudi, wapate kuwa wafalme na makuhani.

294 Utukufu kwa Mungu! Ninajisikia vizuri vya kutosha kunena kwa lugha. Angalia. Tazama. Naam. Inaonekana kana kwamba sina lugha ya kutosha; ningeweza kumsifu kwayo. Ninahitaji moja ambayo hata sijui.

295 Angalia, “Nami nikaangalia . . .” Sikilizeni jambo hili.

Nami nikaona na nikasikia sauti ya malaika wengi . . .

296 Sikilizeni ni yubile ya namna gani inayoendelea! Walipomwona yule Mwana-Kondoo akija na kukitwaa kile Kitabu cha Ukombozi, zile nafsi zilipiga makelele ya furaha. Tutafikia jambo hilo. Wote, kila kitu, wale wazee walianguka chini. Wakamimina maombi ya watakatifu. Ni kitu gani? Kulikuwa na Jamaa wa Karibu aliyetuwakilisha. Walianguka wakasujudu. Nao wakaimba wimbo, na kusema, “Umestahili, kwa maana ulichinjwa!” Angalia kile . . . Na waangalie Malaika hawa!

Nami nikaona na . . . nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi, na za wale wenye uhai, na za wale wazee, na hesabu yao ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi . . . elfu mara elfu, (Whiu! Angalia!)

Wakisema kwa sauti kuu, Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri, na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka.

297 Ni yubile ya namna gani inayoendelea Mbinguni, wakati yule Mwana-Kondoo anapoongoza, anapoondoka kwenye lile jukwaa la uombezi, kuja hapa kutwaa madai Yake!

298 Mwajua, hilo lilimshangaza Yohana sana. Hana budi aliona jina lake limeandikwa pale. Wakati Mihuri hiyo ilipovunjwa, hapana budi alifurahi sana. Sikilizeni yale aliyosema.

Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na upande wa chini ya nchi . . . na vyote . . . ndani ya bahari, na vitu vyote . . . ndani yake, vilivyo ndani yake vilinisikia, nikisema, Baraka . . . heshima . . . utukufu . . . uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondo, hata milele . . . (Amina! Amina, na amina! Loo!)

Na wale wenye uhai wanne wakasema, Amina. Na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka, na wakamsujudu yeye aliye hai milele hata milele.

299 Nena kuhusu yubile, nena kuhusu wakati, wakati huyo Mwana-Kondoo alipotokea! Unaona, kile Kitabu hata kimetiwa muhuri huko Mbinguni, zile siri zimetwiwa muhuri.

300 Unasema, Je! jina langu limo?” Sijui mimi. Ninatumaini limo. Lakini, kama limo, liliwekwa kwenye hicho Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

301 Lakini jambo la kwanza, ambalo liliwakilisha ule ukombozi, alikuja Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naye akakitwaa kile Kitabu, (utukufu!) akakifungua kile Kitabu, na kuichana ile Mihuri, na kukituma duniani, kwa malaika Wake wa saba, kukifunua kwa watu Wake! [Kusanyiko linafurahi sana—Mh.] Haya basi. Loo! jamani! Ni kitu gani kilichotukia? Vigelegele, vifijo, zile haleluya, watiwa mafuta, nguvu, utukufu, dhahirisho! [Kusanyiko linaendelea kufurahi sana.]

302 Na maskini Yohana, aliyekuwa amesimama pale, ndugu yetu, akilia! “Mbona,” yeye akasema, “kila kitu Mbinguni, kila kitu duniani, na kila kitu chini ya bahari, vilinisikia nikisema kwa sauti kuu, ‘Amina! Amina! Baraka, heshima, na uweza, na nguvu, ziwe Kwake Yeye aishiye milele na milele.’”

303 Zungumza kuhusu wakati wa furaha, wakati hiyo Mihuri ilipovunjwa! Yohana hana budi aliangalia ndani na kuona ng’ambo ya pazia la wakati, na kusema, “Yule pale Yohana.” Loo, loo!

304 Alifurahi sana, hata akasema, “Kila kitu Mbinguni.” Hapana budi alisema kwa sauti kuu, sivyo? “Kila kitu Mbinguni, kila kitu duniani, kila kitu chini ya nchi, kila kiumbe, kila kitu kinginecho, vilinisikia nikisema, ‘Amina! Baraka, na utukufu, na hekima, na nguvu, na uweza, na utajiri, ni vyake Yeye.’” Amina!

305 Kwa nini? Wakati ufunuo ulipokuja, ya kwamba yule Mwana-Kondoo, yule Mkombozi, Jamaa yetu, alikuwa amerudi kutoka katika Kiti cha Enzi cha upatanisho na amekwisha toka hapa nje atwae milki Yake. Loo!

Karibuni Mwana-Kondoo atamchukua Bibi-
arusi Wake daima awe ubavuni Pake,
Jeshi lote la Mbinguni litakusanyika;
Loo, litakuwa tamasha lenye utukufu,
watakatifu wote wamevaa nguo nyeupe sana
zisizo na waa;
Nasi tutatawala pamoja na Yesu Milele.

Lo, “Njoo ule,” Bwana aita
(ule Neno), “Njoo ule.”

306 Loo, ni—ni—ninaishiwa na maneno, unaona.

“Njoo ule, njoo ule,”

Unaweza kula mezani pa Bwana wakati wo wote, (Sasa! Lakini wakati atakapoondoka, hakuna tumaini.)

Yeye aliyewalisha makutano, akageuza maji kuwa divai.

³⁰⁷ Yeye aliyesema, ya kwamba, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Loo, jamani! Yeye aliyeahidi mambo haya katika siku za mwisho. Yeye aliyesema mambo haya. Yeye aliye sasa katika wakati wa kufunuliwa kwa mambo haya yanayofanywa wazi. “Njoo ule.” Loo, usikose jambo Hilo, ndugu yangu.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

³⁰⁸ Kesho usiku, kwa neema ya Mungu, tutajaribu kuvunja Muhuri wa Kwanza, kama Mungu atauvunja kwetu na kuturuhusu tuone vile ufunuo huu ulikuwa ni kitu gani, “uliofichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

³⁰⁹ Kabla hatujafanya jambo hilo, ewe rafiki mwenye dhambi, ama mshiriki wa kanisa vuguvugu, je! wewe ni mfuasi tu wa kanisa, ama wewe si mfuasi? Na kama wewe ni mfuasi tu, ni afadhali uliache. Unahitaji Kuzaliwa. Huna budi kuja kwenye ile Damu. Huna budi kuja kwenye kitu fulani kinachoiondolea mbali dhambi tu, mpaka hakuna tena kumbukumbu yake.

³¹⁰ Kama hujafanya matayarisho, bado, kumlaki Mwana-Kondoo hewani! Na kwa mamlaka niliyopewa kwa agizo langu, nililopewa na Mwenyezi Mungu, na kuagizwa na Malaika, Mwali wa Moto, ninawaamuru, katika Jina la Yesu Kristo! Usijaribu kwenda kumlaki na uanachama pekee wa loji la kanisa la dunia hii.

³¹¹ Njoni, wakati Mpatanishi, kadiri nijuavyo mimi, yungali kwenye kile Kiti cha Enzi, akifanya maombezi. Kwa sababu, itakuja siku ambapo mtataka kuja, na hakutakuwako na Mpatanishi. Kwa maana kama tunaona saa tunayoishi, katika wakati wa saba wa kanisa, na siri za Mungu zikiwa jinsi zilivyo, na Roho wa Mungu aliyethibitisha akionyesha kila kitu alichohidi katika siku za mwisho, basi kuna wakati gani zaidi uliosalia? Ewe rafiki mwenye dhambi, njoo.

³¹² Bwana Yesu, majira yanachelewa. Huenda hata ikawa wakati umeenda zaidi ya tunavyodhania. Nasi tunafurahi kuona saa hii ikikaribia. Ni saa yenye utukufu sana ambayo ulimwengu ulipata kujua, kwa ajili ya mwamini. Lakini, kwa mwenye kukataa, ni wakati wa huzuni sana ambao ungeweza kuwako. Hakungepatikana maneno katika alfabeti, herufi za kuandika maneno, ambayo yangeweza kueleza shida na huzuni zilizo mbele. Na wala hakuna maneno ambayo yangeweza kutungwa, kutoka katika alfabeti zetu, kuonyesha baraka zilizo mbele ya mwamini.

313 Baba, huenda kukawa na wengine, usiku wa leo, hapa wasio na tumaini. Nao ni wanadamu wenye akili. Na sasa kama ile Damu ingali iko kwenye Kiti cha Rehema, mruhusu Mwana-Kondoo aondoke kwenye kile Kiti cha Enzi, aingie moyoni mwao, usiku wa leo, na kuwafunulia ya kwamba wao wamepotea. Na kwa mikono iliyojaa Damu, aseme, “Njoo, ikiwa wakati wa kuja ungalipo.”

314 Ninauweka Ujumbe huu, Bwana, pamoja na maombi yangu, mikononi mwako. Fanya lo lote utakalo, Baba, katika Jina la Yesu.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

315 Kama hujatimiza ombi hili na sharti hili! Kama umetegemea tu kanisa lako! Hapakuwepo na kitu cho chote kingaliweza kukomboa. Kama umetegemea maombi ya mtakatifu fulani, ungali umepotea. Kama umezitumainia kazi za mikono yako, jambo fulani ambalo umefanya, matendo mema, umepotea. Kama umetumaini ka—katika maombi ya mama yako, ama haki ya mama yako, baba yako; kama umetumaini katika hilo, umepotea. Kama umetumaini katika miamsho—miamsho fulani ya ajabu, msisimko fulani, wa kunena kwa lugha, ama kucheza dansi! Kama hayo ndiyo tu umetegemea, na humjui yule Mwana-Kondoo, kibinafsi, humjui, basi, ninakuagiza mbele za Mungu, weka sawa jambo hilo, sasa, na Mungu.

316 Ndani kabisa ya moyo wako, omba. Na uwe tu wa kawaida, kwa sababu Mungu hujificha katika urahisi. Unakumbuka, Biblia ilisema, “Wote walioamini waliongezwa.”

317 Na wakati tunapokuombea, ninatumaini ya kwamba utafanya huo uamumzi (wako) mmoja wa Milele, “Bwana, nitasema, ‘Ndiyo!’” Na *uamuzi* ni “jiwe.” Lakini jiwe linafaa nini bila mwashi ambaye anaweza kulichonga, kujenga jengo, lifae kwenye jengo? Basi, acha Roho Mtakatifu akukate kutoka vile ulivyo, akufanye jinsi unavyopaswa kuwa. Kama wewe ni mfuasi tu baridi wa kanisa; kama u mwenye dhambi; cho chote ulicho; kama huna Kristo, bila Roho Mtakatifu, Mungu na akupe amani, usiku wa leo.

318 Sasa, Bwana, nikija kwa akili timamu kabisa kama ni juavyo, na Ki—Kimaandiko sana kama ni juavyo kuja, naja sasa pamoja na hawa niliowakabidhi Kwako, pamoja na Neno. Ninatumaini, Bwana, ya kwamba Neno limepata mahali Pake katika mioyo ya watu, usiku wa leo.

319 Kama kuna kama hao hapa ambao hawajui, ama hawana uhakikisho huo wa Uwepo mtamu wa Roho Mtakatifu ukikaa katika maisha yao; kwamba, hasira, ama kutojali, ama kujipenda, ama cho chote kile kilichokata Kitu hiki kikubwa kutoka kwao, na kimewaweka mbali Nacho; ama kanuni fulani za imani, ama—ama—ama mwamsho fulani, umewaweka mbali

na utamu wa ushirika wa Mungu; ya kwamba sasa kitaondolewa mbali!

³²⁰ Na kwamba huyo Mwana-Kondoo, yule Jamaa aliyeye mtakatifu, aliyelowa Damu, aliyekuja kutoka kwenye kile Kiti cha Enzi, akapitia katika Nuru za Siri za ukumbi wa Kiti cha Enzi cha Mungu, akatoka kwenda kudai urithi Wake! Mungu, jalia, usiku wa leo, ya kwamba wao watampokea. Naomba kila uamuzi ufanywe kwa uchaji, na naomba kwamba wajisalimishe Kwake Yeye peke Yake Ambaye anayeweza kuwakata na kuwafinyanga wakawa wana na binti za Mungu.

³²¹ Sasa, kwa sala ya uchaji, ninafanya jambo hili jinsi ninavyojisikia kuongozwa kufanya. Katika uchaji, mbele za Mungu, kama vile alivyojithibitisha Mwenyewe kwako. Nawe hukuwa Mkristo, ama hukuwa kile tunachoita ninii. . . Si—si— si mwenye kujiunga na madhehebu, lakini ninamaanisha Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Lakini unaamini kwa uchaji Ujumbe huu ni kweli, na unaamini kwa uchaji ya kwamba unaweza tu kuokolewa kwa neema ya Mungu. Nawe unaamini ya kwamba Yeye ananena na moyo wako sasa. Na unataka kumkubali, na uko tayari kwa Neno Lake ku—kukukata kutoka kile ulicho, na kukufanya kile unachopaswa kuwa. Utashuhudia jambo lilo hilo, kwa kusimama kwa miguu yako? Kama mtu huyo yuko hapa, na unataka kuchukua huo msi. . . huo msimamo mkamilifu sana, simama kwa miguu yako.

³²² Baba wa Mbinguni, sijui la kufanya zaidi ila kunukuu Neno Lako. Hawa hapa watu wanaosimama kwa miguu yao, wanaojisikia ya kwamba hawajafika mahali wanapopaswa kuwa, kuwa tayari kwa ajili ya huku Kunyakuliwa, kwa maana kunaweza kutukia kabla ya Muhuri wa Kwanza kufunguliwa kwetu.

³²³ Na, Baba, ninawaombea. Mimi—mimi, kama mtumishi Wako, ninaomba ombi hili kwa yule Mwombezi mkuu, Kristo. Wanapoomba, ninaomba maombi yangu pamoja nao, juu ya kile Kiti cha Enzi cha Mungu cha kipusa, ambapo ile dhabihu iliyolowa Damu imekaa pale usiku wa leo. Na karibu wakati wote huenda akatoka kwenye kile Kiti cha Enzi, kuja kudai mali Yake, ndipo hapana rehema tena iliyosalia; ni hukumu.

³²⁴ Tujalie, Bwana, kwamba watu hawa waliosimama kwa miguu yao, wanaosimama; katika mioyo yao, wakitubu, na wakiwa tayari kumruhusu Roho wa Mungu awafinyange, na kuwakata, na kuwaumba wawe mawe yaliyo hai, wakafanyika Nyumba ya Bwana Mungu. Tujalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako sasa.

³²⁵ Nawe ulisema, “Yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Na sasa Wewe umeketi pale, mbele ya wote, usiku wa leo. Nao wanasimama, wakikukiri Wewe. Na, Bwana, kama jambo hilo

linatoka katika kilindi cha mioyo yao, kwa hakika tu kama vile Neno la Mungu lilivyo halisi, Wewe sasa unawafanyia upatanisho, na kuwakubali katika—katika kiwango cha neema na rehema ya Damu inayosafisha ya Mwana-Kondoo wa dhabihu. Nao watakuwa Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³²⁶ Sasa, ninyi mnaowaona watu hawa waliosimama kwa miguu yao, kijana huyu mwanamume aliye *pale* ndani, na hao wengine wanaosimama, ninyi ambao mlijisikia ya kwamba dhambi yote na hukumu zimeondoka. Ninawatakeni msimame tu, baadhi yenu mlio karibu nao. Wapeni mkono, na kusema, “Ndugu, nitakuwa nikikuombea. Dada, ninakuombea.” Wapeni tu mkono, na kusema, “Mungu akubariki.” Na sasa mengine yamo mkononi mwa Mwenyezi. Sema, “Nitaomba, nami nitafanya yote niwezayo kufanya kuwasaidia kuingia katika Ufalme wa Mungu.”

Loo, huitwa leo!

Loo, Yesu anaita!

Anaita kwa pole akwita leo!

³²⁷ Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Si Yeye ni wa ajabu? [“Amina.”] Loo, tungefanyaje bila Hili? “Mtu hataishi kwa mkate tu; bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, ndivyo mtu atakavyoishi.” Loo, nilishe mimi, Bwana, kwa Neno.

³²⁸ “Msiache kukutanika pamoja, kama ilivyo desturi ya wasioamini, na zaidi sana mnapoona ile Siku ikikaribia.”

³²⁹ Mungu akipenda, kesho usiku, kwa neema ya Mungu, nitajaribu, kwa yote yaliyo ndani yangu, kumwomba Yeye atuombe- . . . atuombee, ya kwamba siri za Mihuri hii, zinapoonekana, zitawatangazia watu Neno la Mungu.

Mpaka nitakapokutana nanyi, Mungu awe pamoja nanyi!

³³⁰ Na sasa namwachia ibada ndugu yetu mpendwa, Ndugu Neville, mchungaji. Ni wangapi wanaompenda Ndugu Neville? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Sasa, sote tunampenda. Njoo huku mbele, Ndugu Neville. Ndugu Neville, Mungu akubariki, ndugu.



UFUNUO WA MIHURI SABA
(The Revelation Of The Seven Seals)

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kutoka tarehe 17 Machi mpaka tarehe 24 Machi, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, na Muhuri wa Saba ukaendelea tarehe 25 Machi katika Hoteli ya Sherwood. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamilifu zaidi, kitabu hiki kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

Haki zote zimewekwa. Kitabu hiki hakiwezi kuuzwa, kuchapishwa tena, ama kufasiriwa katika lugha zingine, ama kutumiwa kwa kuchangisha fedha bila barua ya kuruhusia ya William Branham Evangelistic Association. Kilichapishwa tena katika mwaka wa 2006.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org